# ATHARI ZA KISEMANTIKI KWA WANAFUNZI WAKIKUYU WANAOJIFUNZA KISWAHILI

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY ACQUISITION SECTION P.O. BOX 536, EGERTON
- 1 MAR 2011

NJAU VIRGINIA WANGARI
AM 12/0737/02

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY
EULIB
026 136

Tansifu iliyowasilishwa katika bodi ya shahada za juu katika chuo kikuu cha Egerton ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili katika Kiswahili katika chuo kikuu cha Egerton

CHUO KIKUU CHA EGERTON

2012/89280

NOVEMBA 2008

# UNGAMO NA IDHINI

## UNGAMO

Kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawasilishwa katika chuo kikuu chochote ili kutimiza mahitaji ya shahada yeyote.

SAHIHI ……………………………… TAREHE 28·11·2008……………………………

NJAU VIRGINIA

## IDHINI

Tasnifu hii imewasilishwa katika chuo kikuu cha Egerton kwa madhumuni ya kutosheleza mahitaji ya shahada ya uzamili katika isimu ya Kiswahili kwa idhini na ushauri wetu tulioteuliwa rasmi na chuo kikuu kuisimamia.

1.

Prof. F.O.B. Aswani
Idara ya Lugha isimu na Fasihi
Chuo Kikuu cha Egerton

SAHIHI …………………… TAREHE 28-11-2008……

2. Dkt. C. kitetu
Idara ya Lugha isimu Na Fasihi
Chuo Kikuu cha Egerton

SAHIHI ………………….. TAREHE 2·12·08…………………

**HATILINZI**

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna ruhusa ya kuiga tasnifu hii kwa njia yoyote bila idhini kutoka kwa chuo kikuu cha Egerton au kutoka kwa mwandishi.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

## TABARUKU

Kwa wazazi wangu
Mama Zaweria Nyambura
Baba Peter Njau

Walionilea na kunielimisha
mpaka hapa nilipofika.

## SHUKRANI

Ningetaka kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwa mwenyezi Mungu muumba wa vyote kwa kunineemesha ili niweze kujiendeleza kimasomo. Pia kwa kunijalia siha kuanzia mwanzo hadi mwisho wa masomo yangu. Utukufu wote uwe kwako. Pili, nawashukuru wasimamizi wote na wakuu wa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa fursa ya kujiunga na chuo hiki kusudi nijiendeleze kimasomo. Kama sio idhini yao nisingelipata nafasi hii murua ya kujiimarisha kielimu.

Tatu ningependa kutoa shukrani zangu nyingi kwa Daktari Kitetu kwa jinsi ambavyo amenisaidia kwa hali zote katika kufaulisha masomo yangu. Namshukuru pia kwa kukubali kuwa msimamizi wangu pamoja na mawaidha yake ya kitaaluma aliyonipa ambayo yalielekeza kazi hii. Kutokana na ushauri wake, kazi hii imeweza kufikia kiwango hiki.

Shukrani nyingine za dhati zimwendee Profesa Aswani Buliba ambaye pia kama msimamizi wangu alichangia kuelekeza kazi hii katika hatua zote. Nakuhongera, mwalimu.

Kamwe siwezi kuwasahau walimu wangu wote wa Idara ya Lugha Isimu na Fasihi, Egerton, kama vile Daktari Beja, Daktari Furaha, Daktari Mukuthuria, mabwana Muindi na Mayaka. Nawashukuru sana kwa mwelekeo na elimu mliyonipa. Mlinifaa sana pia katika kunielekeza jinsi ya kuandika na kufanya utafiti.

Nawashukuru pia wanafunzi wenzangu kama vile Mabwana Ontieri, Ngugi, Ng'ethe, Kimani, Mudhune, Bi Ong'au na Nyandiba kwa kunifaa tulipokua tukiendeleza masomo ya shahada hii.

Mwisho nawashukuru aila zangu kama vile mama Bi Zaweria Nyambura, Samuel, John, Simon, dada Margaret, Jane, Miriam na binamu Alex kwa uvumilivu wao wakati nilikuwa nikisoma; walinifaa kwa kila hali na Mungu awabariki.

# IKISIRI

Wanaisimu wa lugha wamefanya utafiti na kuthibitisha kwamba lugha ya kwanza daima huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Iwapo lugha ya kwanza na ya pili ni za jamii moja basi mwanafunzi hufasiri maana na dhana kutoka lugha ya kwanza hadi ya pili. Ingawa Kikikuyu na Kiswahili ni lugha za Kibantu wanafunzi ambao ni wazungumzaji wa Kikikuyu kama lugha ya kwanza hufanya makosa mengi ya kimatamshi na hasa kisemantiki kwa sababu ya athari ya lugha yao ya kwanza. Hakuna utafiti ambao umefanywa kuchunguza jinsi uhamishaji wa maana unavyotokea kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Haswa makosa yanayotokana na uhamishaji huu hayajatambulishwa. Hali kadhalika jinsi maana inavyohasirika kutokana na uhmishaji huu haijachunguzwa. Kutokana na hali hii mtafiti alichunguza na kuainisha makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu kama lugha ya kwanza. Mtafiti alienda hatua mbele na kuangalia jinsi makosa haya yanavyodhihirika katika uandishi wa insha. Alichunguza kiwango cha kuathirika kwa wanafunzi ili aweze kutoa mapendekezo. Utafiti ulifanywa katika wilaya ya Nyandarua ambapo wanafunzi ishirini kutoka shule tano za tarafa ya Ol-kalou, ya wilaya hiyo, waliteuliwa kwa mtindo wa uteuzi huru. Wanafunzi walipatiwa mada tatu za insha waandikie juu yake na maneno kumi ya kutungia sentensi. Hali kadhalika, walipatiwa sentensi kumi wadondoe makosa ya kisemantiki yanayojitokeza. Maneno haya yalitokana na uchunguzi awali uliofanywa na mtafiti. Jumla ya wanafunzi mia moja wazawa wa lugha ya Kikikuyu walitahiniwa. Iligunduliwa kuwa wanafunzi walifanya makosa ya kisemantiki yaliyoathiri maana katika lugha ya Kiswahili. Hii ilitokanaa na tafsiri sisisi, uhamishaji wa maana na ubadilishanaji wa maneno kutoka, lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na ile ya Mkabala wa Urejeleaji Maneno Kijozi zilitumiwa. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Mtafiti aliweza kutoa mapendekezo ya jinsi ya kutatua shida za kisemantiki zinazowatatiza wanafunzi wazawa wa lugha ya Kikikuyu wanapojifunza Kiswahili. Kwamba wanafunzi na walimu waweze kuelewa na kusahihisha makosa yanayotokana na uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya kwanza. Mtafiti amependekeza kuwa walimu na wasomi waelewe kuwa wanafunzi kutoka jamii ya Kikikuyu huwa na shida ya uhamishaji wa kimaana katika lugha ya Kiswahili. Hii itawasaidia kuzua mbinu na mikakati ya kuwasaidia wanafunzi hawa. Pia imependekezwa kuwa mwalimu akiwa darasani awe mwelekezi tu bali muda mwingi uwachiwe wanafunzi ili wafanye mazoezi wao wenyewe.

## ABSTRACT

Various linguists have noted that the first language acquired always affects the learning of the second language. If the second language being learned belongs to the same family with the first language learned, the learners tend to transfer meanings to the second language being acquired. Although Kikuyu and Kiswahili are both Bantu languages, students who are Kikuyu first language speakers make several errors, ranging from pronunciation to semantic ones, due to the first language interference. No study has been conducted on semantic transfer resulting from Kikuyu first language speakers as they learn Kiswahili. Particularly the errors resulting from this transfer have not been investigated. Consequently how meanings in Kiswahili language are affected due to this transfer is still unknown. It is against this background that the researcher, through this study, undertook to investigate semantic errors resulting from Kikuyu students first language speakers as they learn Kiswahili. The researcher went a step further and looked at how these errors are manifested on their written composition. The study also looked at the level of interference on students performance so that recommendations on how to solve this problem can be arrived at. The population was drawn from form three students in Nyandarua district. Twenty students of Kikuyu origin were selected from each school. A total of a hundred students were tested. They were given three topics to write compositions on and were also requested to construct sentences using words provided by the researcher, which were obtained through pilot study. Contrastive Analysis and Word Referent Pairing Approach were used. Data was analyzed using descriptive analysis method after compiling the frequency of mistakes made. It was found that students were transfering meanings from their Kikuyu language to Kiswahili language. This caused them to make errors which affected meanings in Kiswahili Language through direct translation, word substitution and semantic shift. It is anticipated that the findings of this research would go along way in helping students and teachers to understand and correct semantic mistakes resulting from first language transfer. The researcher has made recommendations on the way forward in providing solutions to semantic transfer from Kikuyu first language speakers as they learn Kiswahili. That teachers and instructors handling Kikuyu students first language speakers should be made to know that the said students make semantic mistakes as they learn Kiswahili language. This will help them device methods of assisting them. While in class the teacher should allow students to work on their own as he/she guides them. This will make students practice the skills of Kiswahili language.

**YALIYOMO**


**UKURASA**

**UNGAMO NA IDHINI** ........ ii

**HATILINZI** ........ iii

**TABARUKU** ........ iv

**SHUKRANI** ........ v

**IKISIRI** ........ vi

**ABSTRACT** ........ vii

**YALIYOMO** ........ viii

**DIBAJI YA MAJEDWALI** ........ xi

**SURA YA KWANZA**

**UTANGULIZI** ........ 1

1.1 Usuli wa Mada ........ 2

1.2 Swala la Utafiti ........ 3

1.3 Madhumuni ya Utafiti ........ 3

1.4 Nadharia Tete ........ 3

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 4

1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti ........ 4

1.7 Vikwazo vya utafiti ........ 5

1.8 Lugha ya Kikikuyu na Kiswahili kama Lugha za Kibantu ........ 5

1.9 Hitimisho ........ 7

**SURA YA PILI**

**MAPITIO YA MAANDISHI** ........ 8

2.1 Utangulizi ........ 8

2.2 Maelezo mbalimbali kuhusu dhana ya semantiki na leksia ........ 8

2.3 Makosa yanayotokana na ujifunzaji wa lugha ya pili ........ 13

2.4 Waandishi wa Kiafrika walioandika kuhusu kuathiriana kwa lugha ........ 16

2.5 Misingi ya nadharia ........ 19

2.5.1 Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ........ 19

2.5.2 Nadharia ya Mkabala Wa Urejeleaji Maneno Kijozi ........ 21

2.5.3 Hitimisho ........ 21

## SURA YA TATU


| | | |
|---|---|---|
| | **MBINU ZA UTAFITI** | 22 |
| 3..1 | Utangulizi | 22 |
| 3.2 | Utafiti wa maktabani | 22 |
| 3.2.1 | Utafiti wa nyanjani | 22 |
| 3.3 | Ukusanyaji wa data na uteuzi wa watafitiwa | 23 |
| 3.3.1 | Uteuzi wa Sampuli | 23 |
| 3.3.2 | Ukusanyaji wa data | 24 |
| 3.4 | Mbinu zilizotumika kukusanyia data | 25 |
| 3.5 | Data iliyopatikana | 25 |
| 3.6 | Uchanganuzi wa data | 27 |


## SURA YA NNE


| | | |
|---|---|---|
| | **MATOKEO YA UCHANGANUZI WA DATA** | 28 |
| 4.1 | Utangulizi | 28 |
| 4.2 | Shule ya Upili ya Nyakiambi | 29 |
| 4.3 | Shule ya Upili ya Sabugo | 31 |
| 4.4 | Shule ya Upili ya Mirangine | 32 |
| 4.5 | Shule ya Upili ya Kangui | 34 |
| 4.6 | Shule ya Upili ya Tumaini | 36 |
| 4.7 | Tathmini na matokeo | 38 |
| 4.7.1 | Tafsiri Sisisi | 38 |
| 4.7.2 | Makosa yanayotokana na Uhamishaji wa maana | 39 |
| 4.7.3 | Ubadilishanaji wa Maneno | 41 |
| 4.8 | Umaratokezi wa makosa haya | 42 |
| 4.9 | Chanzo cha makosa | 45 |
| 4.9.1 | Mfumo wa Ngeli katika lugha ya Kiswahili | 45 |
| 4.9.2 | Unyambuaji wa Maneno | 46 |
| 4.9.3 | Uteuzi wa Msamiati Usiofaa | 47 |
| 4.9.4 | Marudio katika lugha ya Kikikuyu | 4 |

## SURA YA TANO

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO** .................................................. 48
5.1 Utangulizi ........................................................................................ 48
5.2 Hitimisho.......................................................................................... 48
5.3 Mapendekezo................................................................................... 48
**MAREJELEO** .................................................................................... 51
Kiambatisho A ....................................................................................... 54
Kiambatisho B ....................................................................................... 55

## DIBAJI YA MAJEDWALI

**UKURASA**


| | | |
|---|---|---|
| Jedwali la 1 | Kielelezo cha jedwali la data ........................................ | 26 |
| Jedwali la 2 | Makosa ya uhamishaji wa kimaana ........................................ | 29 |
| Jedwali 3 | Maneno ya Kiswahili yaliyohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu ........................................ | 30 |
| Jedwali la 4 | Makosa yanayotokana na uhamishaji wa tafsiri sisisi kutoka shule ya upili ya Sabugo ........................................ | 31 |
| Jedwali la 5 | Makosa ya uhamishaji wa kimaana ........................................ | 32 |
| Jedwali la 6 | Sentensi za Kiswahili zilizohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu ........................................ | 33 |
| Jedwali la 7 | Maneno ya Kiswahili yaliyohamishiwa maana kutoka lugha ya Kiswahili katika shule ya upili ya Mirangine ........... | 33 |
| Jedwali la 8 | Makosa ya kiathari ........................................ | 34 |
| Jedwali la 9 | Maneno yanayoonyesha kuathiriwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikikuyu chambilecho uhamishaji na tafsiri sisisi ...... | 35 |
| Jedwali la 10 | Makosa ya tafsiri sisisi vilevile uhamishaji wa kimaana .......... | 37 |
| Jedwali la 11 | Leksia za Kiswahili zilizohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu ........................................ | 37 |
| Jedwali la 12 | Asilimia ya makosa ya tafsiri sisisi ........................................ | 43 |
| Jedwali la 13 | Asilimia ya makosa ya uhamishaji ........................................ | 43 |
| Jedwali la 14 | Asilimia ya makosa ya ubadilishanaji ........................................ | 43 |
| Jedwali la 15 | Tathmini ya jedwali la asilimia moja ya makosa .................. | 44 |

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

Kila lugha ina mfumo wake mahsusi. Katika hali hii mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili huwa na athari ya utamaduni wa lugha yake ya kwanza. Kwa sababu mifumo hii miwili iliyohitilafiana hukutana, hali hii husababisha mivutano ya namna mbalimbali katika vipashio mbalimbali vya lugha. Hivi ni kusema kuwa kuna athari zinazotokana na lugha ya kwanza wakati mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili. Athari hizi zinaweza kuwa za kifonolojia, kisemantiki, kimofolojia au hata za kisintaksia. Katika mkabala huu utafiti huu ulichunguza athari za kisemantiki zinazotokana na lugha ya Kikikuyu kwa mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Hii ni kwa sababu wanafunzi wanaozungumza Kikikuyu kama lugha ya kwanza wamekuwa wakifanya makosa ya kisemantiki wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Makosa haya yamekuwa yakitatiza maana katika lugha ya Kiswahili. Hii inafanya wanafunzi kutojieleza vyema katika lugha ya Kiswahili hasa katika uandishi wa Insha. Hali hii imekuwa ikitatiza umilisi na umahiri wao wa lugha ya Kiswahili wanapojifunza kama lugha ya pili.

Uandishi wa Insha ni miongoni mwa mitihani inayotahiniwa katika kidato cha nne nchini Kenya. Kwa hivyo, wanafunzi wanastahili kurekebishwa wanapofanya makosa. Kutokana na haya, utafiti huu ulifanywa ili kutambulisha na kuainisha makosa ya kisemantiki yanayofanywa na mwanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu anapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Pia ulibainisha jinsi maana katika lugha ya Kiswahili inavyoathirika kutokana na makosa haya ya kisemantiki. Utafiti huu pia ulitathmini kiwango cha kuathirika kwa wanafunzi hawa wa Kikuyu wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Hali hii iliweza kufanyika ili kutoa mapendekezo ya jinsi ya kusuluhisha uhamishaji wa kisemantiki kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

Suala la lugha kuathiriwa na lugha nyingine ni la kijadi. Wanalugha na wanaisimu wengi Chambilecho Johnson (1747), anakiri kuwa haiwezekani kuwa na lugha ambayo haijaathiriwa na nyingine. Hii ni kwa sababu lugha haitokei katika ombwe tupu pasipo kuhusisha binadamu anapojaribu kujiimarisha aushini. Hivyo basi kadri tabia za mwanadamu zinavyozidi kubadilika, na lugha ni hivyo. Maelezo haya yanaelekea kutoa kauli kuwa lugha haiwezi kuthibitiwa kwa kuwapa wanadamu mfumo fulani wa lugha kuufuata. Hii ni kwa sababu tabia na mienendo ya mwanadamu hubadilishwa na kuingiliana kwake na jamii pana ya wanadamu wenzake. Hali hii inafanya lugha moja kuiathiri nyingine.

Ingawa swala la lugha kuathiri nyingine limetafitiwa na wanaisimu wengi kama vile Selinker (1972), Weinreich (1968), na wengine, makosa tunayoyakisia yatafanywa na wanafunzi hawa tuyachukulie kama nadharia tete hadi utafiti kamili ufanywe kuchunguza makosa halisi yanayofanywa na wanafunzi hawa na athari yake kwao. Hii itatusaidia kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na shida hii. Kutokana na haya mbinu na mikakati mbalimbali zitabuniwa ili kusaidia wanafunzi hawa.

Hali hii ilinipa msukumo mkuu na kichocheo cha kutaka kutafiti makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Sikuona utafiti wa awali uliochunguza hali hii. Utafiti huu ulijitokeza kuwa tofauti na wa wanaisimu wengine waliotafiti kuhusu kuathiriwa kwa lugha ya pili na ya kwanza kwa sababu dhana ya uhamishaji kama sababu ya makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza halikuwahi kujitokeza katika tafiti zao. Kile nilichokipata wakati nilipopitia maandishi yao ni kuwa wanadai hakuna anayeweza kukana kuwa lugha ya kwanza huathiri umilisi wa lugha ya pili. Katika kazi hii nimeelezea jinsi athari ya lugha ya Kikikuyu hupelekea mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili kufanya makosa ya kimaana katika lugha ya Kiswahili. Pia, makosa haya yanatokana na nini. Hali kadhalika jinsi ya kutatua shida hizi za kimaana.

## 1.1 Usuli wa Mada

Wanafunzi wa shule za upili nchini Kenya wamekuwa wakifanya vibaya katika lugha ya Kiswahili na walimu wa Kiswahili wamekuwa wakilaumiwa na wakuu wa shule kwa kusababisha hali hii. Katika utafiti huu mtafiti alijikita katika muktadha wa matumizi ya lugha darasani. Ingawa utafiti huu hautashughulikia umenke ilidhihirika kwamba wasichana kufanya vizuri katika mtihani wa Kiswahili kuliko wavulana. Hii ni kwa mujibu wa gazeti la *East African Standard* ya matokeo ya mtihani wa mwaka wa 2003. Hata hivyo utafiti huu haukulenga kuchunguza mtihani wa kidato cha nne lakini ilibainika wazi kuwa mwaka wa 1994 matokeo ya Kiswahili yalirudi nyuma yakilinganishwa na mwaka wa 1993 na hali hii haitii moyo asilani *(Kenya National Examination Council 1997).* Kuna sababu nyingi zilizochangia kutofanya vizuri. Hata hivyo, uchunguzi kamili haujafanywa kuchunguza hali hii. Kwanza wanafunzi hawa hujifunza Kiswahili kama lugha ya pili kumaanisha kwamba yamkini wameathirika kutokana na lugha yao ya kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

Binadamu anapojifunza lugha ya pili huwa anahamisha maumbo na maana kutoka lugha asilia hadi lugha anayojifunza anapojaribu kuelewa lugha hiyo na tamaduni za jamii husika. Mawazo haya yanashikiliwa na mwanaisimu Lado (1957). Naye Selinker (1972), anadai kuwa uhamishaji wa vipengele vya lugha kutoka lugha asilia hadi ya pili huaanzia katika kiwango cha leksia. Ni kutokana na hali hii ambapo mtafiti aliamua kuchunguza makosa yanayosababishwa na mwanafunzi wa jamii ya Kikuyu anapojifunza lugha ya Kiswahili na athari ya makosa haya katika uandishi wa insha. Aghalabu makosa haya husababisha kutofanya vizuri katika mitihani yao. Ingawa makosa wanayoyafanya yamechangiwa na mkusanyiko wa sababau nyingi, ni dhahiri kwamba yamkini baadhi ya makosa ya kisemantiki yaliyokolea yamesababishwa na athari ya lugha ya kwanza.

## 1.2 Swala la Utafiti

Wanafunzi ambao lugha yao ya kwanza ni Kikikuyu hufanya makosa ya kisemantiki yanayotokana na athari ya lugha yao ya kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Makosa haya hutatiza maana na haijulikani ni kwa kiwango gani yanaathiri umilisi wa mwanafunzi wakati anapowasiliana kwa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo utafiti huu ulichunguza makosa na athari hizi na kubainisha ni kwa jinsi gani zinajitokeza katika insha ya mwanafunzi ili kumwelekeza namna ya kuepukana na tatizo hili.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Utafiti huu ulilenga kutimiza malengo yafuatayo:

i) Kuchunguza na kuainisha makosa ya kisemantiki yanayohamishiwa lugha ya Kiswahili na mwanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu anapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili.

ii) Kuthibitisha jinsi maana katika lugha ya Kiswahili inavyoathirika kutokana na makosa haya ya kisemantiki.

iii) Kutathmini kiwango cha kuathirika kwa wanafunzi hawa wa Kikuyu wanapojifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwapa mtihani.

## 1.4 Nadharia Tete

Katika utafiti huu mtafiti aliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i) Mwanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu hufanya makosa ya kisemantiki wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

ii) Makosa ya kisemantiki yanayofanywa na mwanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu hutatiza maana katika lugha ya Kiswahili.

iii) Wanafunzi ambao lugha yao ni Kikikuyu wameathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na lugha yao ya kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa na umuhimu katika taaluma ya elimu na hasa katika lugha ya Kiswahili. Pia, utakuwa na natija katika jamii ya Kikuyu kwa sababu umefanya mtafiti kutoa rai thabiti kwamba wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu huathirika sana na lugha yao ya kwanza, ambayo inawafanya kuwa na makosa chungu nzima ya kisemantiki wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Matokeo ya utafiti huu yatamwelekeza mwalimu kufahamu kwamba wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu huwa na matatizo ya kisemantiki yanayotokana na lugha yao ya kwanza wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Hii itamwezesha kubuni mbinu za kuwasaidia wanafunzi kama hawa. Pia mtafiti ametoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na hali kama hii au jinsi hali hii inavyoweza kurekebishwa. Utafiti huu umechangia katika taaluma ya isimu kwani umebainisha sababu zinazofanya kuweko kwa makosa kama haya kwa mwanafunzi wa kabila la Kikuyu anayejifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Utafiti huu utachochea wataalamu wa isimu kuandika vitabu na makala kuhusiana na mada hii. Matokeo ya utafiti huu pia yatawafaa wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu kwa sababu watafahamu shida zinazowakabili wanapojifunza lugha ya Kiswahili.

## 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti ulifanywa katika wilaya ya Nyandarua kaskazini Wilaya hii ni miongoni mwa wilaya tano katika mkoa wa kati. Wakikuyu wengi huishi katika wilaya hizi; Kirinyaga, Kiambu, Murang'a na Nyeri. Kutokana na haya wilaya hii ilichaguliwa kama sampuli kufanyiwa utafiti. Haingewezekana kufanyia utafiti Wakikuyu wote nchini Kenya. Hii ingechukua muda mrefu zaidi kuliko ilivyotarajiwa. Kikikuyu cha Nyandarua kaskazini kinakubalika na wakikuyu wa wilaya hizo zingine. Utafiti ulifanyiwa nyanjani ambapo shule tano kutoka tarafa ya Ol kalou ya wilaya ya Nyandarua kaskazini ziliweza kuchaguliwa kimaksudi. Shule mbili zilikuwa za bweni na tatu za kusoma mchana na kurudi nyumbani jioni. Katika kila shule wanafunzi ishirini ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kikuyu kama lugha ya kwanza waliweza kuchaguliwa kimaksudi. Wanafunzi wa kidato cha tatu ndio waliofanyiwa utafiti. Katika kiwango hiki ilikisiwa kwamba wao wana ukomavu wa lugha ya Kiswahili. Iwapo bado wanatatizika katika kiwango hiki basi huenda haya ni makosa ambayo yamekolea kutokana na athari ya lugha yao ya kwanza.

Utafiti huu ulichunguza makosa ya kisemantiki yanayofanywa na wanafunzi wa jamii ya Wakikuyu wanapojifunza Kiswahili. Mtafiti alichagua leksia za Kiswahili ambazo zina maana kutoka lugha ya Kikikuyu ambazo mwanafunzi hujaribu kuzifasiri kulingana na lugha

yake mwenyewe. Makosa mengine yalidondolewa kutokana na mitihani mitatu ya insha walizopewa ili waandike. Ingawa lugha ya Kikikuyu huathiri vima vingine vya isimu kama vile fonolojia na mofolojia, utafiti huu ulichunguza taaluma ya Leksia-Semantiki. Hii ni kwa sababu sikuona utafiti wa awali uliochunguza athari za kisemantiki zinazotokana na lugha ya Kikikuyu kwa mwanafunzi wa lugha hiyo anapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Swala la kimaana ni muhimu sana kwa mwanafunzi yeyote anayetaka kuimiliki lugha.

Ingawa semantiki na pragmantiki ni matawi yanayoingiliana mtafiti, hata hivyo, hakujihusisha katika kudadisi uhusiano uliopo kati ya taaluma hizi mbili. Bali azma yake kuu ilikuwa ni kuangalia jinsi maana inavyohasirika kutokana na makisio kwamba hali hii hutokana na kule kuathirika kwa mwanafunzi kutokana na lugha yake ya kwanza. Swala la semantiki ni swala nyeti na linaweza kuzua mijadala na hisia kali kwa vile linahusisha kitivo cha lugha katika ubongo wa binadamu. Hata hivyo, binadamu wa kawaida hana uwezo wa kufahamu kwa kina kinachoendelea katika kitivo hicho ila anaripoti tu yale ambayo anayoyaona na kuyasikia. Kutokana na hali hii, mtafiti alikuwa hana budi kuangalia jinsi mwanafunzi anavyojaribu kujieleza katika lugha ya Kiswahili na aghalabu yale maumbo aliyoyafahamu katika lugha yake ya kwanza yanavyomwathiri anapojifunza Kiswahili.

## 1.7 Vikwazo vya Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na matatizo si haba ambayo yalichangia katika kucheleweshwa kwa kukamilika kwa tasnifu hii. Baadhi ya vikwazo hivi ni kama vile ubovu wa barabara. Wilaya ya Nyandarua imetengwa kimaendeleo kinyume na Wilaya zingine za mkoa wa kati. Barabara hazijawahi kukarabatiwa. Sehemu zingine kama vile Mirangine kuelekea Tumaini hamna barabara ila tu vijia vya miguu. Ilimbidi mtafiti kutumia baiskeli kama chombo cha usafiri licha ya kupitia msituni uliokuwa kimya ila tu wanyama wa mwitu. Tukio hili liliogofya sana. Utafiti huu umechukua muda mrefu sana kukamilika aidha kwa sababu ya kutingika kwa mawasiliano. Kwa mfano tasnifu hii iliwasilishwa katika bodi ya shahada za juu mwaka wa 2005 Aprili na kukwama pale kwa miaka miwili.

## 1.8 Lugha ya Kikikuyu na Kiswahili kama Lugha za Kibantu

Bleek ndiye mwasisi wa dhana Bantu. Kulingana naye lugha za Kibantu huwakilisha lugha zote za Kiafrika zilizoko Kusini mwa jangwa la Sahara. Lugha hizi ni zile ambazo hupanga maneno yake pamoja na majina katika makundi mbalimbali. Makundi haya huwakilisha nomino, pronomino na dhana mbalimbali zinazotumika katika lugha hizo. Lugha hizi ni lugha jumulishi yaani hujumulisha maneno. Huorodhesha majina ya vitu vingi kwa pamoja.

Kwa mfano mtu (umoja) watu (wingi) katika lugha ya Kiswahili *'mundu'* (mtu) umoja na *'andu'* (watu) katika lugha ya Kikikuyu.

Huwa na muundo wa ngeli katika muundo wa lugha hizo kwa mfano lugha ya Kikikuyu na lugha ya Kiswahili huwa na mpangilio wa ngeli kwa mfano ngeli ya a - wa katika lugha ya Kiswahili. Lugha zisizojumulisha vitu hutumia umenke kama njia moja ya kujitambulisha. Hamna umenke katika lugha jumulishi. Sifa nyingine bainifu ya lugha hizi ni kwamba huwa na muundo wa mnyambuliko katika vitenzi vyake. Yaani huweza kurefusha maneno kutokana na shina la neno. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili neno 'piga' laweza kurefushwa kama 'pigia', 'pigisha' 'pigana.' Katika lugha ya Kikikuyu neno *'hura'* laweza kurefushwa na kuwa *'hurira'*, (pigilia) *hurithia* (pigisha) *'hurahura'* (piga piga). Kulingana na Bleek (1862), lugha hizi huwa na mofimu ambayo ina muundo wa 'ba' au 'wa' ambayo huwakilisha mtu au watu ama kundi la watu. Kwa mfano Ba-Hausa kumaanisha watu wa kabila la kihausa, Ba-fulani, watu wa kabila la kifulani. Kuna marudio ya mofimu "Ba' au "wa" katika lugha hizi jumulishi. Kwa hivyo Barth aliunganisha mofimu 'Ba' na *'ntu'* akaunda jina Bantu lililowakilisha lugha jumulishi. Hapo awali kulingana naye lugha hizi zilijulikana kama lugha za 'Ba'. Lugha za Kikikuyu na Kiswahili huwa na sifa bainifu ambazo zimeelezwa hapo juu, kwa hivyo ni lugha za Kibantu. Atkins (1970) anaunga mkono kauli hii. Kutokana na hali hii kuna maingiliano mengi ya kimaana kati ya lugha hizi. Hali hii ilichangia kuwepo kwa makosa mengi yanayotokana na mwingiliano huu yaliyofanywa na wanafunzi wazawa wa lugha ya Kikikuyu wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili.

## 1.9 Hitimisho

Katika sura hii nimeeleza kiini cha utafiti huu hali kadhalika kichocheo kilichomsukuma mtafiti kufanya utafiti. Nadharia tete, umuhimu wa utafiti pamoja na mipaka ya utafiti zimeweza kuelezewa. Katika sura ya pili, inayofuata, mapitio ya maandishi pamoja na misingi ya nadharia zimeweza kufafanuliwa.

## SURA YA PILI

## MAPITIO YA MAANDISHI

### 2.1 Utangulizi

Waandishi mbalimbali wameshughulikia kazi zilizo na ukuruba na hii yangu. Wengi walioandika kuhusu swala la semantiki na Leksia ni wa kutoka nje ya bara la Afrika. Kuna watafiti wengine wa Kiafrika ambao nimerejelea kazi zao. Katika sura hii nimetongoa hoja za wataalamu mbalimbali kuhusu nadharia pana ya Semantiki na Leksia. Pia, athari za kisemantiki zinazofanywa na mwanafunzi kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Ili kupitisha mawazo ya maandishi haya kimantiki vijisehemu mbalimbali vimetumiwa. Katika sehemu ya kwanza nimeelezea maana ya semantiki na jinsi maana inavyojitokeza katika sentensi au katika matini. Katika sehemu ya pili nimeangalia kinachosababisha mwanafunzi kufanya makosa ya kisemantiki anapojifunza lugha ya pili. Katika sehemu ya tatu nimeangalia wandishi wa kiafrika walioandika kuhusu kuathiriana kwa lugha. Sura hii pia ina mdahalo kuhusu misingi ya nadharia iliyosaidia katika kudhibiti maswala ya utafiti huu. Nadharia zilizotumiwa katika utafiti huu ni Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi na ile ya Mkabala wa Urejeaji Maneno Kijozi.

### 2.2 Maelezo mbalimbali kuhusu dhana ya Semantiki na Leksia

Wataalamu wengi wamewahi kufanya utafiti kuhusiana na mada hii ya semantiki na wamesema mengi katika mkabala huu. Postman (1966), anadai kuwa semantiki ni kipengele cha isimu kinachojihusisha na shida za kimaana. Taaluma hii inahusu jinsi mwanadamu anavyopata umilisi wa maana katika lugha. Anadai kuwa binadamu anapata maana ya maneno kwa kuangalia kitendo ambacho mwenzake anakitenda. Kulingana na Ravin (1990), anadai kuwa semantiki lazima ijihusishe na kufafanua baadhi ya vipengele ambavyo havijashughulikiwa na sintaksia pamoja na mofolojia katika sentensi. Kwa hivyo semantiki hufafanua maana katika sentensi ambayo haishughulikiwi katika vima vingine vya lugha.

Mwanalugha Cresswell (1994), asema kuwa kujua maana ya kitu ni kujua ukweli wa jambo hilo. Anadai kuwa iwapo mtu anataka kujua maana ya neno Fulani ni lazima maelezo haya yawe na ukweli ambao unalingana na hali halisi ya ulimwengu. Kwa mfano, iwapo mtu anatamka uneni kunanyesha ni lazima kitendo hiki kihusike na hali ya ukweli hivi kwamba mvua itaonekana ikitiririka au kudondoka kutoka juu. Anadai kuwa maneno ni vipengele muhimu vinavyounga sentensi. Maneno haya lazima yawe na maana inayokubalika. Yaani

ni lazima yasimamie viarifa, vitenzi, nomino, visifa na viungo vingine muhimu vinavyounga sentensi. Hatuwezi kuwa na sentensi pasipo kuwa na maneno ambayo yana maana.

Cruse (1986), anadai kuwa maana ya neno inasemekana kuwa inapatikana kwa namna neno linavyotumika. Anasema kuwa maana hupatikana katika kudhihirisha kwa ishara kile mnenaji anakitaja; kwa mfano, kama anaongea kuhusu 'ng'ombe' anamwonyesha kwa ishara kuwa huyu ndiye mnyama ambaye anamzungumzia. Njia nyingine ya kupata maana ni kusema tu kile ambacho mnenaji anakidhamiria. Maana ya pili hutoa vidokezo vinavyosaidia maana kupatikana na maana ya kwanza huungana na maana ya pili kutoa jawabu kamili. Anasema kuwa ni lazima mnenaji aangaliwe anachokidhamiria katika uneni au neno lake. Hali hii hujulikana kwa kudhania tu. Hii inasaidia mtu kujua kile mnenaji anachokidhamiria. Anadai kuwa maana ya neno hujulikana kwa kulihusisha neno hilo na kitu kinachokaribiana na kile kinachotajwa. Kwa mfano, farasi anahusishwa na punda na hapo maana inaanza kujidokeza na mwishowe maana kamili inapatikana.

Msomi mwingine aliyetia ndaro katika taaluma hii ni Janda (2003) anayedai kuwa maana na maumbo huungana ili maana kamili ya sentensi iweze kueleweka. Leksia hudhaniwa kuwa ni orodha ya maumbomaana ambayo yana uhusiano na kile msemaji anakisema. Licha ya kuwa leksia hutoa maana ya neno, ni lazima vilevile ielezwe jambo Fulani kuhusu sentensi. Ni lazima neno lihusishwe na kile ambacho mnenaji anataka kukisema ili maana ya leksia iweze kujitokeza. Kulingana na nadharia ya utendaji iliyoasisiwa na shule ya wanasemantiki, kila sentensi katika lugha huwa katika hali ya utendaji wa kimaana. Hapa ina maana kuwa, maana hupatikana katika ile hali ya utendaji wa jambo katika tamko.

Chomsky (1981), anadai kuwa lugha ya pili itakuwa na ugumu Fulani katika ujifunzaji wa mwanafunzi ambaye tayari ana umilisi wa lugha ya kwanza. Naye Everson (1994), anakiri kuwa kila uneni una uhusiano na kile kinachotamkwa. Kulingana naye, uneni ni mambo dhahania ambayo mnenaji anayo katika mawazo yake, ambayo anataka kuwasilisha. Anadai kuwa maana ya maneno ni mambo dhabiti ya kisaikolojia; yaani, dhana mbalimbali au, picha zinazopatikana katika ubongo wa binadamu. Kwa hivyo, Semantiki hutegemea saikolojia; tena kuelezea maana ya maneno kunategemea nia ya kisaikolojia ya mnenaji au hali ambazo zina uhusiano na uneni. Anadai kuwa kirejelewa huwa muhimu katika kuelezea maana ya neno kwa sababu kinahusiana na hisia za mwanadamu.

Newmeyer (1993), anadai kuwa mfumo wa kileksia ni mazingira ambapo neno linajipata kwayo na mabadiliko ambayo yanajitokeza. Anadai kuwa semantiki inachangia pakubwa katika kuifanya sentensi yoyote ieleweke na itoe maana mwafaka. Ili sentensi yoyote ieleweke kamili lazima kuwepo na matapo mbalimbali ya kimaana yanayofanya sentensi kueleweka. Mwanaisimu huyu alitambulisha jambo ajenti; yaani anayesababisha jambo kutokea, mada pamoja na chanzo cha jambo, na mwisho malengo ambayo yanastahili kutimizwa ili sentensi iwe kamili. Alisema kuwa sentensi ikiwa na mpangilio mwafaka wa matapo haya, basi maana itaweza kujitokeza murua.

Mwanaisimu mwingine aliyetia hanjamu katika uwanja huu ni Dressler (1988), anayethibitisha kuwa matini huleta maana kwa sababu ya ule mwendeleo wa kuelezea maarifa na maelezo katika muktadha unaorejelewa. Asema kuwa muktadha huo lazima uwe na mwelekeo mwafaka na hali kadhalika uweze kulingana na hali halisi ya ulimwengu. Naye Schmidt (1988), adai kuwa maana katika dhana ni mkusanyiko wa maelezo yanayokubalika. Inadhihirika kwamba kando na tamko au uneni wowote ule mpangilio wa matukio na imani kuhusu jambo au mambo Fulani lazima yawepo ili maana murua iweze kujitokeza katika matini. Wakati watu wanapojieleza katika matini au muktadha wowote ule, dhana na virejelewa vinafanyiwa kazi katika ubongo wa binadamu ambapo hali hii huhifadhiwa. Hali kadhalika, virejelewa hivi na dhana hufanyiwa kazi mara saba kwa wakati mmoja. Hii ndiyo sababu inafanya binadamu kuweza kutoa uneni au kuelewa maana katika muktadha kwa wakati mmoja peke yake.

Wallwork (1985), anadai kuwa binadamu huelewa maana ya maneno kwa kuhusisha neno hilo na kitu Fulani. Kwa mfano, mtalii anayezuru mbuga ya wanyama na akapata neno 'simba' limeandikwa katika mlango atahusisha neno hilo na mnyama anayemwona ndani ya lango hilo na hapo ataweza kupata maana ya neno la mnyama huyo. Anadai kuwa, watu hupata maana ya maneno kwa kuchunguza neno hilo linaashiria nini; yaani, labda neno linarejelea kifaa, kitu au mtu. Anadai kuwa mtoto hupata maana ya maneno kwa kuongezea neno moja au maneno mawili ili kupata maana kamili. Kwa mfano, neno mama huongezwa 'mbaya' kuwa 'mama mbaya.' Hapo, mtoto atakuwa ameunganisha maneno mawili kupata maana. Hii ina maana kuwa neno lolote lile hupata baadhi ya maana yake kutokana na maneno mengine yanayofanana na neno lile. Kwa mfano neno 'basi' si gari ndogo, na si 'motokaa' wala 'trekta' bali ni gari linalobeba abiria wengi na ni kubwa kuliko motokaa.

Mwanaisimu Garman (1994), ameelezea kuwa iwapo mwanafunzi yeyote atataka kupata maana ya neno, basi ataangalia vipengele ambavyo vinajulikana kama visasili ambavyo huunda maana ya kitu kinachotajwa. Mwanafunzi anapounganisha vipengele hivi, anaweza kupata maana ya kitu kinachodhamiriwa. Kwa mfano, kama ni 'kiti' neno hili hugawanywa kuwa ni + kitu kisicho na uhai + kina matendegu + kina sehemu ya kukalia na kadhalika. Upungufu wa kupata maana katika hali hii ni kwamba unaweza kupata kifaa kingine kilicho na maelezo kama haya na hakiwezi kukaliwa au kinaweza kuwa na mahali pa kukaliwa lakini hakina sifa kama zilizoorodheshwa. Kwa mfano, meza ina sifa kama ya kiti kwani inaweza kukaliwa lakini si kiti. Hata hivyo, mtu yeyote anaweza kudondoa maana kwa kuangalia vipengele kama hivi.

Garman (hapo awali)anazidi kufafanua kuwa viwakilishi vya vipengele vya kitu katika ubongo wa binadamu ndivyo humsaidia kupata maana. Kwa mfano, ile dhana mtu aliyo nayo ya mume katika ubongo wa binadamu ndiyo inayomsaidia kuelewa maana yake. Tukifasiri maana ya mume tutaweza kusema + binadamu + mwanamume + ameoa - mwanamke. Hapa, bila shaka msomi yeyote ataweza kuelewa maana ya neno hili na jinsi linavyotumika katika sentensi. Kila neno lazima liwe na kiwakilishi katika kauli ya leksikografia ya ubongo wa binadamu. Hooper na Fraugott (1993), wanadokeza kuwa lazima kuwepo na mipaka kati ya semantiki na pragmantiki ili kuondoa utata kati ya taaluma hizi mbili. Anadai kuwa hata kama tofauti ipo, kwa kiasi, ni mufti kufafanua zaidi mipaka kati ya taaluma hizi ili muktadha wa kile kinazungumzwa ufahamike vyema.

Nao Hurford na Hearsley (1993), wanadai kuwa leksikografia ni kipengele muhimu sana katika kuelezea lugha yoyote ile. Leksikografia murua huwa na vipengele vitatu kuhusu maneno. Neno hilo lazima lielezewe kifonolojia; yaani, jinsi neno hilo linavyoundwa; lazima lielezewe jinsi lilivyopangwa; yaani kipengele cha mofolojia lazima kielezewe vizuri. Pia, anadai kuwa ni lazima lielezwe jinsi msomaji anavyoweza kupata maana ya neno hilo katika sentensi na mwisho mpangilio wa neno hilo katika sentensi lazima lifafanuliwe zaidi. Leksia hiyo lazima ielezewe ina maana gani katika sentensi; hivyo basi, ni lazima neno liwe na maana katika sentensi ili lifahamike vyema.

Mwasisi mwingine aliye na umaarufu mwingi katika kima cha isimu ya lugha ni Chomsky (1970), anayedai kuwa mfumo wa kileksia ulichukuliwa kuwa na viwakilisho kama vifuatavyo + Ajenti; yaani, anayesababisha kitendo kifanyike + mada, yaani, jambo ambalo

linazungumziwa, chanzo; yaani, habari inakotoka na mwishowe mada kuu ili sentensi ikamilike. Kwa mfano, neno mnunuzi lazima lionyeshe vitengo hivi ambavyo vimetajwa. Nani anayenunua, ananua kutoka wapi na nini kinamfanya kununua kitu hicho. Kulingana na nadharia ya semantiki, ni kwamba maana ya usemi ulio na utata hutokana na maana na vipengele katika sentensi na namna vipengele hivyo vinavyounganishwa.

Mwanaisimu mwingine aliyechangia katika taaluma hii ni Newmeyer (1993), anayedai kuwa viwakilisho vya kisemantiki vinaweza kuelezewa kama vipengele ambavyo vinaonyesha vitu katika ulimwengu na mambo au vitu vinavyozungumziwa kuyahusu. Pia, inadaiwa kuwa viwakilisho vya kisemantiki ni mambo yanayotendeka katika ufahamu wa binadamu. Hii ndiyo sababu mtu anapotaja neno 'kuku' haustahili kuwa na kiwakilisho cha neno kuku bali unastahili kuwa na dhana inayoletwa na neno hili. Yaani, katika ubongo mtu atajaribu kuwa na kiwakilisho dhabiti cha huyo ndege. Mwanafunzi anapokuwa akijifunza lugha ya pili huwa anatawaliwa na kanuni iliyoasisiwa na mwanaisimu Chomsky (1981), inayodai kuwa kuna mambo ya kidhahania na ya kiisimu ambayo yanahusika na lugha zote za kiasili. Kanuni hizi zinadai kuwa hali awali ya mawazo au akili ya mnenaji wa lugha ya kwanza huchangia pakubwa katika umilisi wa lugha ya kwanza. Hali hii dhahania huweza kumtatiza mwanafunzi anapojaribu kumiliki lugha ya pili.

Dixon (1992), anadai kuwa katika kiwango cha semantiki maneno yanaweza kupangwa katika vipengele vilivyo na maana sawa katika sentensi. Anasema kwamba katika kiwango cha sarufi, maneno yanaweza kupangwa katika vikundi ambavyo vinajulikana kama matamshi ya maneno. Naye Radford (1992), anaongezea kuwa, kila neno au leksia lazima idhihirishe hilo neno liko katika tapo gani au ni neno la kiwango kipi katika leksikografia. Kila neno lazima lielezwe vizuri kama ni nomino au ni kitenzi. Hapa, msomi yeyote ataweza kuchanganua vyema neno analolitafitia ili kupata maarifa anayohitaji.

Msomi mwingine anayejulikana kama Mulligan (1990), anadai kuwa iwapo mzungumuzaji atanuia kuzungumza na mwenzake, lazima mawazo yale anayotaka kuwasilisha yawe yamehifadhika katika ubongo wa binadamu ili kuwe na mawasiliano barabara. Anadai kuwa ni lazima kuwepo na kiwakilishi hasa cha kile kinachotajwa na mzungumzaji wakati anapotoa uneni. Anadai kuwa, anapoelezea hali hii, ni lazima aonyeshe kuwa kitendo anachokitaja kinalingana na hali halisi ya maisha. Kwa mfano, uneni 'kunanyesha' unadhihirisha hukumu yangu kamili kuwa kitendo cha kunyesha kinatendeka. Mzungumzaji

anapotoa kauli kama hii, basi hapo hutoa kauli yake iliyo na uhakika kwa kweli kunanyesha kwa vile itakuwa inaonekana wazi kuwa kitendo kile kinafanyika. Anadokeza kuwa, iwapo ni lazima kuwe na mawasiliano na maelewano, ni lazima kuwepo na mawazo pamoja na uhakika wa kile ambacho uneni unataka kuwasilisha. Hapa, yule anayesikiliza ataweza kuelewa kile anachotakikana kufanya. Kwa hivyo, tendo hilo litalingana na muktadha wa hali halisi ya maisha kwa sababu kutakuwa na uhakika wa kitendo hicho. Anaema kuwa ni lazima ishara itumike ili msikilizaji aweze kufahamu vyema viwakilishi vilivyomo katika ubongo wa binadamu anapotajiwa neno, tendo au kitu.

## 2.3 Makosa yanayotokana na Ujifunzaji wa Lugha ya Pili

Katika sehemu hii nimeonyesha kwa nini wanafunzi hufanya makosa wanapojifunza lugha ya pili kwa kuzingatia kazi za wataalamu mbalimbali. Odlin (1994), anadai kuwa wakati wanafunzi wanakutana na matumizi ya maneno yasiyofanana na lugha yao asilia, wao hudhania maana yake. Odlin (hapo juu) anadai kuwa maneno ambayo hufanana katika lugha asilia hutafsiriwa vilevile katika lugha ambayo mwanafunzi anajifunza. Isitoshe, uhusiano kati ya maana ya leksia na ya sentensi huungana pamoja na kuunda maana ya semantiki. Lado (1957), anadai kuwa sio wazungumzaji wote wa lugha watakuwa na ugumu ulio sawa katika kujifunza lugha. Anadai kuwa orodha ya makosa yanatokana na athari ya lugha ya kwanza kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili lazima yachukuliwe kama nadharia tete hadi utafiti halisi ufanywe kwa kuangalia matamshi hasa kutoka kwa wanafunzi wazungumzaji wa lugha yenyewe. Katika utafiti huu, mtafiti hatakuwa na budi kuingilia swala la homonimu kwa sababu makisio ya mtafiti ni kwamba maneno ya Kikikuyu yanayobeba maana zaidi ya moja humfanya mwanafunzi kukanganyika anapojaribu kuyafasiri katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na maoni ya Ingram (1994), mwanafunzi anapotumia homonimu hudhania kuwa maana ya maneno haya huwa sawa na hapo ndipo anapofanya makosa anaposhindwa kupambanua hali hii.

Halliday (1975), anadai kuwa mwanafunzi anapoelewa maana ya neno hujaribu kulifasiri katika ubongo wake hivi kwamba wakati anapokuwa mkomavu akijifunza lugha ngeni hujaribu kuhamisha maana aliyonayo katika ufahamu wa ubongo wake na hapo atakuwa na matatizo anapojifunza lugha geni. Hii ni kwa sababu tayari amehifadhi maneno yale katika ubongo wake na kujaribu kuingiza maneno mengine mapya kunaleta utata. Kulingana na maoni ya Dixon (1992), neno linaweza kuwa na maana mbili tofauti. Kwanza linaweza kuwakilisha kurejelewa na vilevile linaweza kusimamia hisia ambapo neno linawakilisha

uhusiano uliopo kati ya neno na neno lingine. Maana vilevile inatokana na jinsi maneno yameunganishwa pamoja kuleta maana ya sentensi, kishazi au kielezi. Goldsmith (1995) anaunga mkono kauli hii.

Maana inapatikana wakati mnenaji anapochagua maneno ambayo yataungana pamoja kuleta maana fulani mwishoni mwa sentensi au neno au pia usemi atakaoutamka. Katika maana lazima sarufi izingatiwe; vilevile lazima hali iangaliwe jinsi mambo haya mawili yatakavyokuwa na uhusiano. Katika Lugha yeyote ile lazima sarufi na maneno yahusishwe ili kukamilisha sentensi. Ikiwa mzungumzaji yeyote atakutana na neno geni anapojifunza lugha ya kwanza, hujifunza maana ya neno hilo halafu baadaye anajaribu kulitumia katika lugha ambayo anajifunza. Ikiwa mwanafunzi atasikia neno geni mara ya kwanza atajaribu kulihusisha na kile anachokijua ambacho kinakaribiana na neno hilo, kisha mara moja ataweza kung'amua maana ya neno lenyewe.

Kauli ya mwanaisimu Thomas (1995), imetia nuru katika kazi hii. Anadai kuwa maneno hubadilika maana kwa mwanafunzi anayejaribu kukopa msamiati wa lugha asili ili ayaingize katika lugha ya pili anayojifunza. Anaelezea kuwa iwapo lugha haina msamiati wa kutosha basi lugha hiyo hujaribu kuiga maneno ya mkopo hasa iwapo lugha inayokopwa ina hadhi katika jamii. Kwa kuwa mabadiliko hutokea kati ya jamii basi lazima tofauti hii ya mazungumzo iwe kwa sababu ya mazingira na kitamaduni. Hii ndiyo inapelekea kusababisha mnenaji mmoja kuwa na uzungumzi tofauti na yule mwingine. Mabadiliko yanapotokea katika usemi lazima yahusishe wazungumzaji wote wanaoshiriki. Hivi ni kusema kwamba wao lazima waelewane jinsi ya kupashana mazungumzo haya. Kulingana na maoni ya Selinker (1972), hata ingawa wazungumzaji watapatikana kuwa na makosa fulani katika lugha makosa haya hubadilika kutoka mzungumzaji mmoja baada ya mwingine kwa sababu makosa watakayosababisha ni tofauti baina ya mwanafunzi mmoja na yule mwingine. Hali hii inaelezea kwa nini mwanafunzi hufanya vyema kuliko mwingine.

Kulingana na maoni ya Allwright (1991), makosa yanayopatikana darasani yanaweza kuwa yanatokana na kutokuwa na umahiri wa lugha. Anasema yanajulikana kama makosa ya umahiri. Hii mara nyingi hutokea iwapo maneno yanakaribiana au yanaelekea kuwa na uhusiano wa karibu. Kulingana na mwanaisimu huyu, neno huweza kupatikana kuwa limeelezewa vibaya ikiwa halikuchaguliwa vyema katika leksikografia ya mnenaji. Hali hii hutokea hivi kwamba msemaji hujipata amebadilisha neno na lingine kimakosa kulingana na maoni ya Corder (1981),

Adai kwamba makosa ni mambo yanayotokea mara kwa mara katika
lugha ambayo yanafanywa na mwanafunzi anayejifunza lugha ngeni na ambayo hayafuati kanuni au sheria za lugha hiyo.

Tofauti za kimazingira na kitamaduni huchangia pakubwa katika kuonyesha jinsi wanafunzi watakavyoelewa lugha darasani. Lass (1991), Adai kuwa tofauti katika matamshi husababishwa na mazingira ambayo mzungumzaji anatoka, hali hii huchangia pakubwa katika kuonyesha jinsi leksia zitatamkwa kwa njia tofauti na mara nyingine husababisha makosa ya kisemantiki. Kila mnenaji huonyeshwa upekee wake katika kutamka na kuelezea leksia katika mazingira yanayomkabili.

Odlin (1994), aligundua kwamba msamiati mwingi unaoundwa na mwanafunzi ukiwa na uhamishaji maneno ya lugha ya kwanza katika sehemu za Afrika Magharibi, hutokea kwa sababu ya athari ya maingiliano ya lugha. Katika hali hii inadhihirika kuwa kila mtu huwa na mpangilio wa maneno yake katika leksikografia yake na huweza kuwasilishwa kwa njia tofauti na mtu mwingine. Hali hii vilevile huchangiwa na uana, kiwango cha jamii na vilevile mtindo wa lugha wa kila binadamu. Kadri walivyo tofauti ndivyo kutakuwa na ubobeaji wa matumizi ya lugha na uchaguzi wa maneno. Mnyambuliko ni hali ya kurefusha neno kwa kuongezea viambishi katika shina la neno. Mwanafunzi huweza kunyambua neno bila kuzingatia sheria zinazohitajika anaposhindwa kupata msamiati ufaao. Ikiwa neno litakuwa na mabadiliko basi neno hilo huwa limepitia katika mfanyiko unaojulikana kama badiliko la kileksia. Hapa, neno linajulikana kupoteza baadhi ya viungo vyake kwa sababu ya upekee wa watu na vilevile ule umilisi wao wa maneno au leksia katika lugha.

Wanafunzi huweza kubadilishana maneno iwapo maneno yanakaribiana lakini yana maana tofauti kabisa. Iwapo mtu anataka kutumia neno moja kwa mfano huweza kulifanya litamkike tofauti ili lisije likamkanganya katika kuleta maana anayoitarajia. Kule kuathiriana kwa lugha na nyingine husababisha kuwe na mabadiliko ya Leksia. Hii husababisha upekee wa kimazingira na maumbo na mambo yaliyorithiwa kutoka kwa jamii na yule mwenye kuzungumza. Matamshi ya mtu binafsi huchangia pakubwa katika kuonyesha ubadilikaji wa maneno pamoja na sauti.Hata wakati mwingine mzungumzaji huweza kufinyanga maneno ili yaweze kuwa na mwelekeo ambao yeye anautaka katika sentensi zake. Neno hubadilika kulingana na mazingira ambapo neno hilo linatumika. Muktadha huweza kufanya neno likabadilika kwa jinsi ambayo linatumika. Matini inayokaribiana huweza kuchangia katika

kuwepo kwa mabadiliko ya maneno katika lugha. Istiara huchangia sana katika kuleta mabadiliko katika lugha. Haya ni maoni ya Ingram (1994).

Wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili hufanya makosa mengi ya kimaana kwa sababu ya kuathiriwa na lugha yao ya kwanza. Ajabu ni kwamba wanafunzi huwa mara nyingi hawajui kuwa wanapotoka hadi warekebishwe na wale wanaowasikiliza ambao hawana athari hiyo. Makosa haya yanayofanywa na wanafunzi darasani yanatokana na kutokuwa na umilisi wa lugha wanayojifunza. Hata yanajulikana kama makosa ya kutokuwa na umahiri wa lugha. Haya ni kwa mujibu wa Alwright (1989). Kile kinachotendeka ni kwamba mwanafunzi hujaribu kufasiri mtindo wa kimaana wa lugha ya pili kutokana na lugha yake ya kwanza. Mara nyingine mwanafunzi huunda neno bila kuzingatia sheria maalum zinazohitajika. Aghalabu hufanya hivyo anapolemewa na msamiati wa maneno katika lugha ya pili anayojifunza. Anapofanya hivyo huweza kusababisha makosa ya kimaana katika lugha ya pili anayojifunza.

Wakati mwingine mwanafunzi huweza kufinyanga maneno ili yaweze kuwa na mwelekeo ambao yeye binafsi anautaka katika sentensi zake. Hali hii pia huweza kusababisha makosa ya kimaana katika lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza.Hata hivyo, kuna baadhi ya wanaisimu kama vile Corder (1981), wanaodai kuwa uhamishaji wa maumbo yanayopatikana katika lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza huweza kuchukuliwa kama hatua kabambe ambazo mwanafunzi anazichukua katika kujaribu kuratibisha data ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Kulingana na mwanaisimu Lado (1957), lazima mwanafunzi aangaliwe kutokana na ufahamu kwamba anao uwezo wa kuhamisha maumbo ya lugha yake ya kwanza hadi lugha ya pili ambayo anajifunza. Uhamishaji huu huwafanya wanafunzi kusababisha makosa katika lugha ya pili wanayojifunza. Anasema kwamba lugha ya kwanza huchukuliwa kama kigezo au kielelezo cha kutabiri makosa ambayo mwanafunzi atayafanya katika lugha ya pili ambayo anajifunza.

## 2.4 Waandishi wa Kiafrika walioandika kuhusu kuathiriana kwa lugha

Wataalam wengi wa lugha waliobobea katika uwanja huu, kutoka bara la Afrika wameandika kuhusu jinsi lugha za kiafrika zinavyoathiri au kuathiriwa na lugha za Kiingereza na Kiswahili. Mathalan Mosha (1971), alichunguza maneno ya Kiswahili na Kiingereza yaliyokopwa na lugha ya Kiganda. Mwanalugha huyu alishughulikia athari hizi katika vima vya kifonolojia na mofolojia. Katika tathmini yake alitilia mkazo kuwa lugha za Kiafrika

sharti zikope ili kukabiliana na hali ya mpito ambayo inahitaji waafrika kubadilisha mifumo yao ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ili iwiane na msukumo wa mahitaji ya kisiasa. Ingawa utafiti wake unatofautiana na huu wangu, kwa jinsi ambavyo unahusu ukopaji maneno ni wazi kuwa maelezo haya yalichangia katika upanuzi wa maarifa katika kazi hii.

Mukuthuria (2004), katika tasnifu yake aliangalia kuathiriana kwa lugha ya Kitigania na Kiswahili. Alipochanganua data yake aligundua kuwa mifumo ya kifonolojia ya lugha hizi mbili, Kitigania na Kiswahili inatofautiana kwa upande wa fonimu zinazotumiwa, japo ni za Kibantu. Tofauti hizi ndizo zinaleta athari katika ngazi ya fonolojia. Hii ilibainishwa na dosari nyingi za kitahajia zilizopatikana katika insha zilizokuwa zimeandikwa na wanafunzi wa asili ya Tigania. Kwa mfano badala ya kusema /pamba/ Watigania hutamka /bamba/ /bahati/mbahati/.

Anasema kuwa maumbo ya Kitigania yaliathiri lugha ya Kiswahili kwa mfano /nga /limanga,/ kupiganga/. Katika maelezo yake anakiri kuwa utamaduni una upekee na ndiposa athari nyingi za lugha zinasababishwa na tofauti za utamaduni. Isitoshe asema kuwa lugha za Kiafrika zina upekee wake kwa jinsi ambavyo zinaathiriana na lugha ya Kiswahili. Ingawa kazi hii imetia natija katika tasnifu hii, kazi ya Mukuthuria ni tofauti na hii yangu. Hii ni kwa sababu msomi huyu ameangalia kuathiriana kwa lugha mbili; Kitigania na Kiswahili. Kazi hii inahusu lugha ya Kiswahili kuathiriwa na lugha ya Kikikuyu. Yaani jinsi mwanafunzi mzungumzaji wa lugha ya Kikikuyu kama lugha ya kwanza anavyopata kuathiriwa anapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Isitoshe Mukuthuria anaangalia kuathiriana kwa lugha hizi mbili katika kiwango cha mofolojia na fonolojia. Kazi hii ilichunguza kuathiriwa kwa lugha ya Kikikuyu katika kima cha leksia-semantiki.

Watafiti wengine walioandika kuhusu lugha za Kiafrika ni kama vile Rubanza (1979). Utafiti wake ulikuwa juu ya mahusiano kati ya Kiswahili na Kihanya. Alisema kuwa Kiswahili kimeathiriwa na lugha ya Kihanya kwa sababu ya kutumika katika mazingira mamoja. Alipendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusina na swala hili.

Mochiwa (1979), alitafiti athari za Kiswahili katika Kizigua nchini Tanzania. Aligundua kuwa lugha ya Kizigua imeathiri Kiswahili katika ngazi ya fonolojia, mofolojia na sintaksia. Aligudua kuwa maingiliano ya lugha mbili yangeweza kuzua athari ya lugha dhidi ya

nyingine. Kazi hii imekuwa na umuhimu kwa hii yangu kwa kiasi kwa sababu inahusu lugha moja kuiathiri nyingine. Tofauti ni kuwa kazi yangu inashughulikia kima cha kisemantiki.

Nurse (1980) alizingatia suala la kihistoria alipokuwa akiandika utafiti wake kuhusu kuathiriana kwa lugha za kibantu na lugha za kigeni. Alisema kuathiriana kunaweza kuwa kwa msamiati, mofolojia au fonolojia. Alisema kuwa wazungumzaji wa lugha mbili wanapokutana kuathiriana kunatokea.

Kariuki (2000), ameshughulikia jinsi wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu wanapojifunza Kingereza wanapata kuathirika. Ingawa utafiti huu hauhusiani moja kwa moja na utafiti wangu ni wazi kuwa utafaa kazi hii. Hii ni kwa sababu alichunguza iwapo lugha asilia huathiri umahiri wa lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza.

Komunte (2001) alifanya utafiti akijaribu kuangalia chanzo cha matokeo mabaya nchini Tanzania. Aligundua kuwa kuathiriana kwa lugha ndiko chanzo cha matokeo mabaya katika mitihani ya kingereza. Aligundua kuwa chanzo cha kuathiriwa kwa lugha ya kingereza kulitokana na hali ya kufanya Kiswahili kuwa lugha rasmi, na lugha ya kufundishia kuanzia mwaka wa 1967. Pia, uwingi- lugha kwa upande wa walimu na wanafunzi kulichangia kuzorotesha umilisi wa lugha ya kingereza. Utafiti huu ulifaa tasnifu hii kwa sababu ulibainsha jinsi maingiliano ya lugha mbili yanavyopelekea wanafunzi kuathiriwa wanapojifunza lugha ya pili.

Kuna hali ambazo zinazoshurutisha Kiswahili kukopa maneno kutoka kwa lugha nyingine. Hii ni kutokana na haja ya mtaji wa kutimiza uanishaji na ufafanuzi wa dhana ngeni za asasi za kisiasa, kijamii, na kiuchumi pamoja na matumizi ya Kiswahili kwa wingi. Hali hii hufanya maneno ya Kiswahili kurudiwarudiwa. Kwa mfano, na vyombo vya habari. Hali hii pamoja na kuzuka kwa taalumu za kigeni ambazo hazikuwepo zamani ndio Mwaro (2000) anarejelea kama ukopaji. Ambao unatokana na kutokuweko kwa msamiati asili wa kurejelea dhana mpya inayoingia katika lugha pokezi. Taaluma za kigeni zinasaidia msamiati wa lugha ya kigeni kupenya katika lugha pokezi ili kuziendeleza. Lugha pokezi hukopa leksia za kigeni ili fahiwa yake ieleweke vyema. Jambo hili aghalabu husababisha lugha ya Kiswahili kuathiriwa na lugha zingine.

### 2.5 Misingi ya Nadharia

#### 2.5.1 Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi

Katika utafiti huu mtafiti aliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi. Nadharia hii ilianza kufanyiwa utafiti katika mwaka wa (1940), na miaka ya sitini. Waasisi wa nadharia hii ni kama vile Lado, Selinker; Weinrich na wengine. Nadharia hii inadai kuwa lugha ya kwanza daima huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili. Hii ni kwa sababu mwanafunzi huhamisha maumbo ya lugha yake asilia hadi lugha ya pili anapojaribu kuelewa lugha hiyo na tamaduni zake. Haya ni kwa mujibu wa Lado (1957). Vilevile inadai kuwa maumbo yaliyo magumu kuelewa katika lugha ya kwanza yatakuwa magumu kuelewa katika lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza. Kama maumbo ni rahisi katika lugha ya kwanza pia yatakuwa rahisi kuelewa katika lugha ya pili ambayo mwanafunzi anayojifunza. Nadharia hii pia inadai kuwa kama lugha ya kwanza na ya pili zinafanana kutakuwa na kuathiriana kwa lugha hizi mbili.

Lado (hapo awali), anadai kuwa binadamu huhamisha maumbo na maana pamoja na mpangilio wa mfumo wa lugha kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ambayo anajifunza anapojaribu kuelewa tamaduni za jamii inayohusika. Anasema kuwa ni lazima mwanafunzi aangaliwe kutokana na ufahamu kwamba anao uwezo wa kuhamisha maumbo ya lugha yake asili hadi lugha ya pili ambayo anajifunza. Anasema kuwa mwalimu anaweza kutabiri ruwaza na mpangilio wa maneno yatakayomletea mwanafunzi shida na ule ambao hauwezi kumletea shida yeyote anapojifunza lugha ya pili.

Lado (1957), anadai kuwa ni lazima kuwe na ulinganifu wa lugha ya kwanza na wa lugha lengwa ili kuelewa vyema makosa yatakayojitokeza. Anadai kuwa maumbo yanayofana na lugha ya kwanza yatakuwa rahisi kuelewa kwa mwanafunzi anapojaribu kuelewa lugha ya pili na yale ambayo hayafanani na ya lugha ya kwanza yatakuwa magumu kuelewa. Maoni haya yaliungwa mkono na Klein (1986). Weinreich (1968), anadai kuwa, kadri lugha zilivyo tofauti ndivyo kutakuwa na ugumu katika ujifunzaji wa lugha hiyo na jinsi zilivyofanana, ndivyo itakuwa rahisi kuelewa lugha hiyo. Anadai kuwa kama lugha mbili zinafanana kutakuwa na uhamishaji wa maumbo na kama ni tofauti kutakuwa na kuathiriana kwa lugha hizi mbili. Kulingana na Selinker (1972), makosa ambayo tunayafikiria au tunayaona yakifanywa na wanafunzi wa jamii Fulani wanapojifunza lugha ya pili tuyachukulie kama nadharia tete hadi utafiti kamili ufanywe kuhusiana na makosa maalum yanayofanywa na wanafunzi hao.

Weinreich anadokeza kuwa ili kuelewa vyema makosa yatakayojitokeza wakati wa kujifunza lugha ya pili itambidi mwalimu kuwa na mpangilio na sheria za mfuatano wa maneno ili kuweza kulinganisha lugha ya kwanza na lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza. Alionyesha kwamba wazungumzaji wa lugha ya kwanza ambao muundo wa lugha yao haumbatani sambamba na wa lugha ya pili inayosomwa walionekana wakiwa na uhamishaji wa data ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Weinreich anadokeza kwamba mwanafunzi hutumia mfumo wa lugha ya kwanza kujielezea katika lugha ya pili ambayo anajifunza.

Haya ni baadhi ya mabadiliko ambayo mwanafunzi hujaribu kukabiliana nayo wakati anajifunza lugha ya pili. Selinker (1972), anadokeza kwamba wakati mwingine mwanafunzi anaweza kuhamisha maumbo kutoka lugha lengwa hadi lugha ya kwanza. Hali hii inajulikana kama kuathiriana kwa kinyume. Weinreich anadai kuwa maumbo ya sauti yanayoonekana kufanana katika lugha huweza kuwa tofauti lugha mbili au zaidi zinapolinganishwa. Anaendelea kudai kuwa uhusiano uliopo kati ya mofimu na sarufi ya lugha moja inaweza kuendelezwa katika maongezi ya lugha nyingine hali ambayo aliita uazimaji wa maneno. Isitoshe uhamishaji wa maumbo huweza kutokea kutokana na hali ambayo mwanafunzi huweza kufikia ukaribu wa lugha ya kwanza na lugha ya pili.

Selinker (hapo awali), adai kuwa ni vigumu kuwa na uwili lugha pasipokuwa na mwingiliano wa mpangilio wa maneno kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Hata hivyo hamna mwanafunzi yeyote ambaye anaweza kuhamisha mofolojia yote ya lugha ya kwanza kwa kuitafsiri au kuazima maneno katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Vilevile yale maumbo yanayohamishwa hufanywa hivyo kwa uteuzi. Freeman na Long katika Odlin (1994), walidai kuwa makosa yaliyotokana na athari ya lugha ya kwanza yalibadilika kutoka utafiti mmoja hadi mwingine. Weinrech (1968), aliibuka na hali ambayo inajulikana kama kilele cha ukomavu wa lugha. Hali hii inadokeza kwamba kuna hatua ambayo mwanafunzi anafika ambapo hawezi kurekebika katika ujifunzaji wa lugha. Yaani kufikia wakati huu atakuwa amehifadhi sheria zote za lugha ya kwanza na itakuwa vigumu kurekebisha makosa anayofanya. Kulingana na Ferguson (1989), kuna maumbo yenye kurudiwa ambayo yanadhihirika wakati mwanafunzi anamiliki maumbo ya kifonolojia katika lugha ya kwanza.

Waasisi hawa wanadai kuwa wakati mwingine maumbo ya lugha au mfumo uliofanana wa lugha si sababu ya kuwepo kwa urahisi katika ujifunzaji wa lugha. Yaani hata kama lugha zinakaribiana mara nyingi haimaanishi kuwa hiyo itakuwa sababu ya mwanafunzi kuelewa

lugha hiyo ya pili anayojifunza barabara. Utafiti wa wanafunzi wa kijapani elfu mbili mia tano ulipofanywa uligundua kuwa nadharia hii ya ulinganuzi ilipungukiwa katika kutabiri kiwango cha kuathiriana. Waligundua kwamba maumbo yaliyokaribiana na lugha ya kiingereza hayakuwa rahisi kujifunza. Nadharia hii ilimfaa mtafiti kwa sababu alichunguza kuathiriwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikikuyu. Pia inaonyesha uhamishaji wa maumbo haya ya kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili wakati mwanafunzi wa Kikuyu anapojifunza Kiswahili.

### 2.5.2 Nadharia ya Mkabala Urejeleaji Maneno Kijozi

Ili kudhibiti maswala ya kisemantiki mtafiti alitumia mtazamo wa Mkabala wa Urejeleaji maneno Kijozi. Mtazamo huu uliasisiwa na Schlesinger (1982), na unakita katika dhana kuwa binadamu hupata umilisi wa lugha kwa kuhusisha dhana hiyo na maneno yanayorejelewa. Dromi (1987), kwa kuyapambanua mawazo ya Schlesinger (1982), anadokeza kwamba katika hali halisi ya maisha, watoto wanaojifunza lugha hutangamana na tajriba mbalimbali. Kutokana na tajriba hizi ndipo wakaweza kujenga maana ambazo wao huzihusisha na hali mbalimbali wanazokumbana nazo. Mtazamo huu wa Schlesinger unatokana na maoni ya Augustin kama anavyonukuliwa na Dromi (1987), kwamba kila neno linawakilisha kirejelewa kimoja. Mtazamo huu unafaa kupambanua maswala ya homonimu. Neno la Kikuyu 'ikia' huwakilisha kutupa na kusukuma. Ni kutokana na hali hii ambapo mtafiti ananuia kutumia mtazamo huu kuchanganulia maswala mbalimbali ya kisemantiki.

### 2.5.3 Hitimisho

Katika sura hii mengi yanayohusiana na dhana ya semantiki na leksia yamejadiliwa. Isitoshe sababu mbalimbali zinazopelekea mwanafunzi kuwa na makosa ya kiathari anapojifunza lugha ya pili zimeweza kuelezewa. Hali kadhalika kuna maandishi ya baadhi ya waandishi wa kiafrika waliotafitia lugha tofauti tofauti za kibantu kuhusiana na swala hili la kiathari. Zaidi ya haya maelezo kuhusu nadharia zilizoteuliwa ili kufanikisha utafiti huu zimeweza kujadiliwa. Nadharia ya Uchanganuzi Linganuzi ilitumiwa kwa sababu inaruhusu ulinganishaji wa mifumo miwili ya lugha ili kubainisha tofauti za lugha hizo. Kwa hivyo, ilisaidia kubainisha ulinganifu na tofauti zinazosababisha athari kati ya lugha ya Kikikuyu na lugha ya Kiswahili. Nadharia ilitumika kwa mwegemeo wa Weinreich (1968) anayedai kuwa iwapo lugha zinafanana kutakuwa na athari pamoja na uhamishaji wa maumbo. Nadharia ya Mkabala wa Urejeleaji Maneno Kijozi ilifaa katika kupambanua maswala ya leksia. Sura inayofuata inaonyesha jinsi data iliyokusanywa na kuchanganuliwa.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Katika sura hii mbinu zilizotumiwa kukusanyia data zimeonyeshwa. Utafiti ulifanywa katika wilaya ya Nyandarua. Sampuli ilipatikna katika tarafa ya Ol Kalou. Wanafunzi wa kidato cha tatu ndio waliofanyiwa utafiti. Hii ni baada ya kudhibitisha kuwa wao ni wazawa wa lugha ya Kikikuyu. Hii ni kwa sababu walionekana wakiwa na umilisi wa lugha kwa kuzungumza Kikikuyu kwa njia ya ufasaha. Walimu wa shule walisaidia katika kutambulisha wanafunzi hawa. Data ilipatikana kwa kuwapa wanafunzi mada tatu waandike insha juu yake na pia maneno yaliyobeba maana ya Kikuyu yaweze kutumiwa katika sentensi za Kiswahili. Pia walipewa sentensi zilizoandikwa vibaya ili wanafunzi waweze kuzisahihisha. Hatua hizo zimeelezewa katika sura hii. Data ilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya kimaelezo kama inavyoelezewa na Bryman (1994), Kothari (2002) na Seliger na Schohammy (1990) baada ya kuona makosa yaliyofanywa na wanafunzi.

## 3.2 Utafiti wa maktabani

Utafiti ulifanywa kwa njia mbili; utafiti wa nyanjani, na utafiti wa maktabani. Maktaba ambazo zilifanyiwa utafiti ni kama vile maktaba ya Jomo Kenyatta chuo kikuu cha Nairobi. Maktaba ya Moi katika chuo kikuu cha Kenyatta. Maktaba ya chuo kikuu cha Egerton. Katika utafiti wa maktabani maarifa zaidi yaliongezewa. Hasa kuhusiana na kazi ambazo zimechunguza jinsi lugha ya kwanza inavyoathiri ujifunzanji wa lugha ya pili kitaalam. Makala mengine yaliyohusiana na taaluma hii yaliweza kundondolewa kutoka mtandaowazi katika tarakilishi.

### 3.2.1 Utafiti wa Nyanjani

Utafiti ulifanywa katika Wilaya ya Nyandarua kaskazini Shule zilizoshirikishwa ni shule za upili za Nyakiambi, Sabugo, Tumaini Kangui na Miragine. Shule za kata ya Ol Kalou ndizo zilizoteuliwa. Wanafunzi wa kidato cha tatu ndio walioshirikishwa. Utafiti huu ulikusanya data ya maandishi kutokana na mada tatu za insha wanafunzi walizopewa kuandika juu yake. Wakati wa kusahihisha kazi hii, mtafiti aliangalia makosa yanayotokana na uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Yaani; makosa ya kuathiriwa kwa lugha ya Kiswahili kimaana na lugha ya Kikikuyu. Makosa mengine yalidondolewa kutokana na maneno ambayo wanafunzi walipewa na Mtafiti. Maneno haya yalibeba leksia za Kikikuyu *(Rejelea kiambitisho B).* Wanafunzi waliagizwa kuyatungia sentensi. Mtafiti aliangalia iwapo mwanafunzi atapotoka na kuhamisha maana ya lugha ya Kikikuyu iliyopo

katika leksia hizi katika lugha ya Kiswahili. Makosa yaliyopatikana yalichangia data ya Mtafiti. Wanafunzi pia walipewa sentensi ambazo zilikuwa na mushkeli wa kimaana. Mushkeli huu ulitokana na uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Mtafiti aliangalia iwapo mwanafunzi atatambua kuwa sentensi alizopewa zilikuwa na ila. Mwanafunzi alistahili kutambua na kubainisha makosa haya. Iwapo hangetambua makosa yaliyokuwepo katika sentensi hizi, jambo hili lilionyesha kuwa alikuwa amathirika sana.

## 3.3 Ukusanyaji wa data na uteuzi wa watafitiwa

Wilaya ya Nyandarua kaskazini ndiyo iliyochaguliwa kufanyiwa utafiti. Wilaya hii ni mojawapo ya Wilaya tano za Mkoa wa kati. Idadi kubwa ya waakaji wa wilaya hizi ni wa kabila la Kikuyu. Wilaya hii ina upekee kwa jinsi ambavyo ina wakikuyu waliohama kutoka Wilaya hizo zingine za Mkoa wa kati. Yaani, utapata wakikuyu kutoka wilaya za: Nyeri, Murang'a, Kiambu na Kirinyaga. Kikikuyu cha Nyandarua kaskazini ndicho kilichofaa zaidi kwa sababu kinakubalika kwa Wakikuyu wote kutoka Mkoa wa Kati. Wilaya hii ina takriban shule mia moja za sekondari. Shule tano ndizo zilizoteuliwa ili kufanyiwa utafiti.

### 3.3.1 Uteuzi wa Sampuli

Tarafa ya Ol Kalou ilichaguliwa kwa sababu shule nyingi za upili katika Wilaya ya Nyandarua kaskazini zinapatikana katika eneo hili. Wakaaji wengi wa sehemu hii ni wazawa wa lugha ya Kikikuyu. Hali hii ilimsaidia Mtafiti katika kuwatambua wanafunzi ambao asili yao ni kabila la Kikuyu na wana umilisi wa lugha hiyo. Kwa hivyo lugha yao ya kwanza ilikuwa ni Kikikuyu. Hata hivyo mtafiti aliwauliza wanafunzi wajitambulishe. Wakati walikuwa wakiwasiliana, ilikuwa shahiri dhahiri kwa kweli asili yao ni kabila la Kikuyu. Changamoto inayowakumba wazungumzaji wazawa wa kabila la Kikuyu ya matamshi mabaya ya kutotofautisha kimadede 'r' na 'l' ilikuwa thibitisho ya kutosha. Katika kujieleza kwao hungekosa kujua kuwa wao ni wahasiriwa wa lugha ya Kikuyu kwa jinsi ambavyo walikuwa wakihamisha maana kutoka lugha yao ya kwanza hadi lugha ya Kiswahili. Waalimu wa Kiswahili pamoja na kaimu wa mwalimu mkuu wa shule walisaidia mtafiti pia katika kuwatambulisha wanafunzi wa asili ya lugha ya Kikikuyu. Wanafunzi ishirini ishirini kutoka shule tano waliweza kuteuliwa kwa mtindo wa uteuzi huru. Jumla ya wanafunzi mia moja walitahiniwa. Wanafunzi wa kidato cha tatu ndio walioteuliwa. Katika kiwango hiki mwanafunzi amefikia kiwango cha ukomavu wa lugha.

Iwapo bado anatatizika katika kiwango hiki, basi haya ni makosa ambayo yamekolea kutokana na lugha ya kwanza ambayo ni Kikikuyu.

### 3.3.2 Ukusanyaji wa data

Hatua ya 1: Mada wanazopewa wanafunzi kuandika juu yake mara nyingi huwa ni maswala ibuka. Ndiposa Mtafiti akachagua mada hizi. Mada hizi zilikuwa zinashawishi mwanafunzi kutoa maelezo kwa kina. Kutokana na haya makosa mengi yaliweza kujitokeza. Wanafunzi walipewa mtihani uliokuwa na mada tatu ambazo waliagizwa kuandika insha juu yake. *(Rejelea kiambatisho A).* Insha ya kwanza ilikuwa ya kimaelezo; *'Hatua ambazo serikali yapaswa kuchukua kufufua uchumi wa nchi hii.'* Kwa kawaida wanafunzi wanapojaribiwa hasa katika mtihani darasani au ule wa mwisho wa kidato cha nne, huagizwa kuandika mada zilizo na masuala ibuka ya sampuli hii. Hapa mwanafunzi ataonyesha umahiri wake wa lugha kwa jinsi ambavyo atatongoa na kujadili hoja baada ya nyingine. Hali hii ilimsaidia sana mtafiti kwa sababu wakati mwanafunzi alikuwa akijadili hoja zake athari za kisemantiki zilizotokana na lugha ya Kikikuyu ziliweza kujitokeza na kudondolewa. Yaani maana ilivyojitokeza katika matini mwanafunzi alipokuwa akijielezea.

Insha ya pili ilikuwa ya methali *'Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe'.* Katika mitihani shuleni na ya kitaifa mwanafunzi huagizwa kuandika insha ya methali. Mwanafunzi hupimwa kiwango chake cha kujieleza kwa njia ya ufasaha. Hii ni kwa sababu insha ya methali inamlazimisha kuelezea kisa kinachooana na kichwa cha methali aliyopewa kwa njia yenye ustadi na ufasaha. Insha kama hii pia hupimwa ubunifu wa mwanafunzi anapojieleza. Wanafunzi walipokuwa wakiandika insha kuhusu methali hii makosa mengi ya kisemantiki kutokana na lugha ya kikuyu yaliweza kujitokeza. Hii ni kwa sababu kadri mwanafunzi alivyojieleza kwa kina, ndivyo makosa mengi ya kimaana yalivyojitokeza. Hii ilichangia data ambayo mtafiti aliitazama.

Insha ya tatu ilikuwa kuhusu hotuba. *'Jinsi ya kuimarisha usalama katika kata yako.'* Wanafunzi huagizwa kuandika kuhusu insha za hotuba mara kwa mara shuleni, katika mitihani ya mijarabu shuleni na hata mtihani wa mwisho wa kidato cha nne. Insha za aina hii hutarajiwa kupima kiwango cha ukwasi wa lugha kwa mwanafunzi. Pia watahini huangalia uasilia wa mawazo wakati mwanafunzi anapoandika hotuba yake. Wakati anapojieleza ndivyo umaarufu wake wa lugha unavyojidhihirisha. Wakati mwanafunzi alikuwa akijieleza makosa mengi ya kisemantiki yaliyotokana na athari ya lugha ya Kikuyu yaliweza
kudondolewa. Aghalabu wanafunzi wanapoagizwa kuandika insha hushauriwa wasiandike maneno chini ya kiwango cha mia tatu. Maneno ya kiwango hiki yangempa mtafiti data

aliyokusudia. Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi, mtafiti aliweza kurekodi alama za wanafunzi ili kuchanganuliwa baadaye.

### 3.4 Mbinu zilizotumika kukusanyia data

**Hatua ya 1:** Mtafiti aliwapa wanafunzi mtihani uliokuwa na insha tatu ambapo waliagizwa waandike insha hizo kulingana na maagizo. *(Rejela kiambatisho A).* Mtafiti aliweza kusahihisha kazi hizo huku akidondoa makosa ya kisemantiki yanayojitokeza. Aliwatuza wanafunzi na kurekodi alama za kila mmoja ili kuchanganuliwa baadaye.

**Hatua ya 2:** Mtafiti aliwapa wanafunzi maneno kumi ambayo yamebeba leksia ambazo zimehamishwa kutoka lugha ya Kikikuyu na kuingizwa katika lugha ya Kiswahili, pia waliweza kupewa maneno kumi waeleze mushkeli uliomo katika sentensi hizo. *(Rejelea kiambatisho B).* Mtafiti alisahihisha kazi hiyo huku akidondoa makosa ya semantiki yaliyojitokeza na kuweza kurekodi alama zao. Maneno haya yalimpa mtafiti data iliyokusudiwa.

### 3.5 Data iliyopatikana

Data iliyopatikana ilitokana na makosa ya kisemantiki yaliyopatikana kutoka uandishi wa insha. Makosa haya yalitokana na athari ya lugha ya Kikikuyu kwa mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Makosa mengine yalipatikana baada ya kusahihisha sentensi zilizokuwa na mushkeli wa kimaana. Pia kuna makosa yaliyopatikana baada ya wanafunzi kupewa maneno na kuulizwa watunge sentensi. Sentensi zilizoonyesha kuwa mwanafunzi ana athari ya lugha ya kwanza ziliweza kutambulishwa. Mtafiti alitumia kielelezo hiki ili kufasiri data vizuri. Haingewezekana kuandika data yote iliyopatikana katika jedwali hili. Mtafiti amenakili mifano michache iliyotokana na usahihishaji data ilipokuwa ikichanganuliwa. Kielelezo hiki kilikusudiwa kumwelekeza yeyote anayesoma kufahamu data iliyopatikana na jinsi ilivyochanganuliwa.

**Jedwali la data la 1 Kielelezo cha Jedwali la data**

| **Jina la shule. Mfano: Nyakiambi** | **Makosa ya kisemantiki. Mfano:** | **Matapo ya makosa haya. Mfano: Uhamishaji wa kimaana** |
|---|---|---|
| 1. Insha | Serikali inafinyilia watu wake | Makosa haya yanatokana na uhamishaji wa maana kutoka lugha ya Kikikuyu. *'Thirikari nirahinyiriria andu ake'* |
| | Siwezi kutupa wakati na watu kama nyinyi | Maana imehamishwa kutokana na lugha ya Kikikuyu *'ndingite mathaa makwa na andu ta inyui'* |
| | Alitaka kujitengenezea maisha | Maana imehamishwa kutoka lugha ya Kikikuyu *'gwithondekera uturo'* |
| 2. Sentensi zilizokuwa na mushkeli wa kimaana | Alienda hospitali kutengenezwa kichwa kilichokuwa kinamuuma | Maana inayojitokeza katika sentensi hii inaonyesha kuhamishwa kwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu iliyo na kauli ya matibabu *'Agithii thibitari guthondekwo'* |
| | Watu walijitolelea | Maana inatokana na lugha ya Kikikuyu *'kwirutira'* haya ni makosa ya uhamishaji maana. |
| 3. Maneno yaliyokuwa na athari ya lugha ya Kikikuyu. | Wewe ndiwe ulituma nichelewe | Neno 'tuma' latokana na leksia ya Kikikuyu *'tuma'* kwa maana ya kusababisha katika lugha ya Kiswahili. Katika Kiswahili sanifu hatuwezi kusema 'ulituma nichelewe.' |
| | Toa: Anatoa kazi katika upelelezi wa jinai | Neno hili limehamishwa kutokana na *'ruta'* katika lugha ya Kikikuyu kwa maana ya kufanya katika lugha ya Kiswahili. |

## 3.6 Uchanganuzi wa Data

**Hatua ya Kwanza:** Baada ya kupitia kazi ya kila mwanafunzi na kuona makosa ya semantiki aliyoyafanya mtafiti aliyainisha na kuyaweka katika matapo mbalimbali kisha aliweza kuyafafanua huku akithibiti nadharia tete kwa kutumia data alizopata. Mtafiti aliweza kuzifasiri kwa kutumia mbinu ya kimaelezo. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya kuangalia umaratokezi wa makosa yaliyofanywa, kisha alichanganua ni asilimia ngapi ya wanafunzi walio na matatizo haya baadaye aliweza kutoa uamuzi mwafaka.

**Hatua ya 2:** Ili kuthibitisha kwamba wanafunzi hawa wameathirika sana mtafiti alitumia asilimia kama kigezo cha kupimia hali hii. Aliyaweka makosa haya kati ya wanafunzi aliowatahini na kupiga mara mia moja yani:

$$\frac{X}{100} \times 100$$

X inawakilisha aina ya makosa kwa mfano uhamishaji na kadhalika.

100 inawakilisha idadi ya wanafunzi.

100 inawakilisha asili mia ya wanafunzi.

Matokeo ya hesabu hii yaliweza kumsaidia mtafiti kuona ni makosa gani yaliyokolea kisha aliyaweka katika grafu kwenye mihimili ili kufasiriwa vyema na kutoa mapendekezo ya jinsi ya kukabiliana na shida hizi. Mtafiti aliweza kuelezea makosa haya yanatokana na nini.

# SURA YA NNE

## MATOKEO YA UCHANGANUZI WA DATA

### 4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliweza kuchanganua data na kutoa maelezo kutokana na data hiyo aliyoipata. Data ilichanganuliwa kwa kuorodhesha makosa mbalimbali yaliyofanywa na wanafunzi kutoka shule tano zilizochaguliwa. Makosa haya yalidondolewa kutoka uandishi wa insha kwa mintarafu ya majedwali katika faslu hii. Pia kutokana na sentensi walizopewa wachanganue na maneno watunge sentensi. (*Rejelea kiambatisho A na B*). Makosa waliyofanya yalitokana na athari ya lugha ya Kikikuyu kwa mwanafunzi anayejifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Makosa yameonyeshwa na kujadiliwa kutoka shule tano zilizoteuliwa na mtafiti. Ili kutoa ithibati zenye mashiko nadharia ya uchanganuzi linganuzi na ile ya mkabala wa Urejeleaji Maneno Kijozi zilitumiwa ili kuonyesha kwa nini makosa haya yanatokea.

Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi ilidhihirika kuwa wanafunzi wameathirika kwa kiwango kikubwa na lugha yao ya kwanza. Hii iliwasababisha kutofanya vyema katika mitihani mbalimbali waliyopewa na mtafiti. Katika usahihishaji wa insha, makosa mengi kama vile ya uhamishaji, udhanifu na ubadilishanaji yalijitokeza. Makosa haya yamejadiliwa vyema kwa kupitia shule baada ya nyingine. Hali hii imeonyeshwa vyema katika sehemu ya 4.0.2 hadi 4.0.6. Makosa haya yanathibitisha kuwa wanafunzi kutoka jamii ya Wakikuyu hufanya makosa ya kisemantiki wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili. Makosa haya yamewekwa katika matapo mbalimbali katika sehemu ya tathmini na matokeo. Ili kuonyesha kiwango cha kuathirika mtafiti ameweza kuonyesha umaratokezi wa makosa waliyofanya. Kati ya wanafunzi mia moja waliofanyiwa utafiti asilimia hamsini walionekana kuwa na makosa yaliyotokana na uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Asilimia arobaine na sita walikuwa na makosa ya ubadilishaji wa maneno kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Hali hii imewasilishwa vyema katika sehemu ya 4.2 inayoonyesha umaratokezi wa makosa. Katika sehemu 4.3 mtafiti ameonyesha makosa haya yanatokana na nini. Mtafiti aliweza kuainisha shule baada ya nyingine ili kuonyesha mufti jinsi makosa haya yalivyojitokeza.

## 4.2 Shule ya Upili ya Nyakiambi

Katika shule hii ya wasichana ya Nyakiambi mtafiti alipowapa wanafunzi mtihani alipata kuwa wanafunzi hawa walikuwa tofauti kidogo na shule zingine za sehemu hii. Makosa waliyoyafanya hayakuwa mengi sana sawia na shule zingine za hapa. Lakini jambo la kushangaza ni kwamba makosa yaliyojitokeza kitovu chake ni sawa na makosa ya wanafunzi wengine yaani athari ya lugha ya kwanza.

Shule hii ni ya wasichana peke yake. Wasichana walionekana wakifanya vyema kuliko wavulana ingawa mtafiti hakuwa akishughulikia swala la umenke, ilijitokeza tu. Hata hivyo kuna makosa ya tafsiri yaliyojitokeza vilevile ya ubadilishanaji na yale ya uhamishaji. Ifuatayo ni ratiba ya makosa yaliyojitokeza katika shule hii.

**Sentensi zilizopatikana na makosa**

Makosa haya yanatokana na uhamishaji wa maana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 2 Makosa ya uhamishaji wa kimaana**

| **Sentensi zilioandikwa kimakosa** | **Tafsiri ya sentensi hizi katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Mtu yule alifutwo kazi. | *Mundu uria niarafutirwo wira.* | Mtu yule alifutwa kazi. |
| Alitegwo na mawe akaanguka. | *Niarategirwo ni ihiga aragwa.* | Alijikwaa |
| Watu walijitolelea. | *Andu nimarerutiire* | Watu walijitolea |
| Kunipea. | *Kuhe* | Kunipatia |
| Juhudi zetu zitatupa. | *Mauthi maitu nimaratuheire* | Juhudi zetu zitatupatia |
| Serikali imefinyilia watu. | *Thirikari nirahinyiriirie andu.* | Serikali inagandamiza watu. |
| Kuliendelea hivyo. | *Gugithii uguo* | Hali hiyo iliweza kuendelea hivyo. |
| Hivyo ni kuonyeshana. | *Uguo ni kuonania* | Hivyo ni kuonyesha |
| Alipiga nguo. | *Niarahurire nguo* | Kuosha nguo |

**Yafuatayo ni maneno yaliyopatikana na makosa**

Makosa haya yanabainisha jinsi mwanafunzi anapoeleza maana ya maneno akiwa ameathiriwa na lugha yake ya Kikikuyu. Makosa yanatokana na uhamishaji wa maana.

**Jedwali la 3 Maneno ya Kiswahili yaliyohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu**

| **Maneno yaliyotumiwa vibaya** | **Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Kusondeka | *Guthondeka* | Kutengeneza |
| 'Tupa'<br>Alikuwa akipita akanitupa. | *Ekuhitukaga anjikia.* | Alikuwa akipita akanisukuma |
| 'Unda'<br>Undia Simon nyumba ya mbao. | *Turira Simon nyumba ya mbao.* | Jengea Simon nyumba ya mbao. |
| 'Enda'<br>Endeni muoshe mikono. | *Thiii mwithambe moko* | Endeni mnawe mikono. |
| 'Shika'<br>Alishika gredi ya chini katika mtihani. | *Anyitire ngirindi ya thi kigeranioini.* | Alipata gredi ya chini katika mtihani. |

Hivi ni kuonyesha kuwa wakati mwanafunzi anapojifunza lugha ya pili hujaribu kuelezea maana kutokana na ufaahamu alio nao wa lugha ya kwanza. Kulingana na Weinreich (1968), ambaye ni mwasisi wa nadharia ya uchanganuzi linganuzi anadai kuwa hali hii hutokea wakati mwanafunzi anapojaribu kuelewa lugha ya pili na tamaduni za lugha hiyo. Hii ndiyo sababu tunaona mwanafunzi akiwa amenaswa na hali hii kisha akaweza kufasiri maana kulingana na ufahamu wa lugha yake ya kwanza. Mtafiti aligundua kuwa wanafunzi walichanganyikiwa walipokuwa wakisahihisha sentensi zilizobeba leksia za Kikikuyu. Kwa mfano wengi wao hawakuona tofauti iliyokuwa kati ya kusema alipiga nguo na kuosha nguo. Mwanafunzi anaposema kupiga nguo huweza kutinga maana hivi kwamba Kiswahili sanifu kinahasirika. Kitendo cha kupiga ni kama vile kuchuka mti na kuweza kuugongesha juu ya kitu kingine. Basi mwanafunzi anaposema kupiga nguo hii haina fahiwa kabisa katika Kiswahili sanifu. Haya ni badhi ya makosa yanayotokana na uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili. Mtahini wa kazi hii popote alipo atatatanika katika Kiswahili kama hiki. Kutokana na matokeo haya utafiti ulidhihirika kuwa mwanafunzi

huhifadhi msamiati wa lugha yake ya kwanza na anautumia katika kujielezea katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Nadharia ya uchanganuzi linganuzi inadai kuwa mwanafunzi huwa anahamisha maana na maumbo kutoka lugha yake ya kwanza hadi lugha ya pili ambayo anajifunza. Hii ndiyo sababu iliyofanya wanafunzi kupatikana wakiwa na makosa mengi.

## 4.3 Shule ya Upili ya Sabugo

Shule ya upili ya Sabugo ni shule ya mseto yaani wavulana na wasichana husoma kwa pamoja. Kazi za wanafunzi hawa ishirini ziliweza kusahihishwa na makosa mbalimbali yaliweza kujitokeza. Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi hawa mtafiti aligundua kuwa hata kama mwanafunzi amefikia ukomavu wa lugha katika kidato hiki cha tatu bado hajapata ule umilisi wa lugha unaohitajika. Hii ni kwa sababu lugha ya kwanza imemwathiri sana.

**Haya ndiyo baadhi ya makosa yaliyokolea katika kazi za wanafunzi hawa**

Makosa haya yanaonyesha uhamishaji wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Mengine yanaonyesha tafsiri vilevile.

**Jedwali la 4 Makosa yanayotokana na uhamishaji wa tafsiri sisisi kutoka shule ya upili ya Sabugo**

| Sentensi zilizoandikwa kimakosa | Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu | Kiswahili Sahihi |
|---|---|---|
| Mamangu alipata mtoto kwa kuchinjwa | *Niarathinjirwo akiheo mwana.* | Alipata mtoto kwa njia ya upasuaji. |
| Siwezi kutupa wakati na watu kama nyinyi. | *Ndingite mathaa makwa na andu ta inyui.* | Siwezi kupoteza wakati wangu na watu kama nyinyi. |
| Ninaanzia kwa kusema kuwa | *Ndirambiriria na kuuga uu* | Ninaanza kwa kusema kuwa |
| Wanaenda kutoa vita kwao. | *Magithii kuruta mbaara kwao* | Kwenda kusababisha vita kwao. |
| Akamwambia aingie ndani atoe mavazi ya nyumba. | *Akimwira aingire thiinii arute nguo cia nyumba* | Akamwambia aingie ndani atoe matandiko ya nyumba. |
| Serikali haisikii huruma kwa watu. | *Thirikari ndiiguagira andu tha.* | Serikali haihisi huruma au haiwahurumii watu wake. |
| Serikali ikataze vitu vinavyoletwa huku nchini. | *Thirikari igirie indo iria irarehwo guku bururiini.* | Serikali ikataze vitu vinavyoletwa hapa nchini. |

Maneno yaliyoandikwa vibaya kwa sababu ya athari ya lugha ya Kikikuyu kwa mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 5 Makosa ya uhamishaji wa kimaana**

| Maneno yaliyoandikwa vibaya | Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu | Kiswahili Sahihi |
|---|---|---|
| 'Tuma'<br>Wewe ndiwe ulituma nichelewe | *Wee niwe utumire njererwo* | Wewe ndiwe ulisababisha kuchelewa kwangu. |
| 'Piga'<br>Alikuwa akipiga nguo | *Ekuhuraga nguo* | Alikuwa akiosha nguo |
| 'Shika'<br>Je ulishika vile ulivyoambiwa | *Niunyitire uria wirirwo* | Je ulielewa vile ulivyoambiwa |
| 'Sikia'<br>Ninasikia njaa | *Nindiraigwa ng'aragu* | Ninahisi njaa |

Wanafunzi walionekana kuwa na makosa mengi ya kimaana hata mengine ya mianzo mibaya kwa mfano 'ninaanzia kwa kusema kuwa'. Hii ni kutokana na athari ya lugha ya kwanza waliyonayo. Kwa mfano katika lugha ya Kikikuyu wanasema *'ndirambiriria na kuuga uu'* Hali hii inadhihirisha kuwa wamehifadhi msamiati wa lugha yao ya kwanza na wanatumia dhana hizo kujielezea katika lugha ya pili. Corder (1981), anadai kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi wanapojieleza katika lugha ya pili yanatokana na hali ya kutaka kuratibisha data ya lugha ya kwanza katika lugha ya pili.

## 4.4 Shule ya Upili Mirangine

Shule hii ya Mirangine ilidhibitisha kuwa kwa kweli wanafunzi wa shule hii wameathirika kutokana na lugha yao ya kwanza. Shule hii ni ya mseto na wanafunzi huenda shuleni asubuhi na kurudi makwao jioni. Wanafunzi hawa walionekana na makosa yaliyoonyesha kuwa hawana ukomavu wa lugha unaohitajika katika kiwango hiki cha kidato cha tatu. Walionyesha kuhifadhi msamiati wa lugha yao ya kwanza. Yaani lugha yao ya Kikikuyu. Walikuwa wakihamisha maana, dhana na maumbo ya lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Haya ni baadhi ya makosa yaliyojitokeza wakati kazi za wanafunzi hawa zilipokuwa zikisahihishwa.**

Makosa haya yanaonyesha athari ya lugha ya Kikikuyu katika kuelezea maana ya sentensi katika lugha ya Kiswahili. Dhana ya uhamishaji imejitokeza katika makosa haya.

**Jedwali la 6 Sentenzi za Kiswahili zilizohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu**

| **Sentensi zilizokuwa na makosa** | **Tafsiri ya sentensi hizo katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Kuosha mikono | *Guthambia moko* | Kunawa mikono. |
| Walipoenda sokoni waling'ang'ania wakatiwe pesa. | *Mathii thoko maruire matinirio mbia.* | Waling'ang'ania wakatiwe bei. |
| Kenya na Uganda walichapana. | *Kenya na Uganda nimarahuranire* | Kenya na Uganda walipigana. |
| Ambia Mary aje ajioge. | *Ira Mary oke ethambe.* | Ambia Mary aje aoge |
| Mamangu amekomboa nyumba katika mtaa ule. | *Mami niarakomborire nyumba mutaa uria.* | Mamangu amepanga nyumba mtaa ule. |
| Nilikuwa nimeinamilia pale mpaka nikachoka. | *Nguinamiriire haria nginya ndanoga.* | Nilikuwa nimeinama pale mpaka nikachoka. |
| Mamangu ameenda kufungwa nywele. | *Mami arathire kuohwo njuiri.* | Mama aliendа kusukwa nywele. |
| Kushika samaki | *Kunyita thamaki* | Kuvua samaki. |

Haya ni makosa yanayoonyesha jinsi mwanafunzi alivyoathiriwa na lugha ya Kikikuyu anapojifunza lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 7 Maneno ya Kiswahilil yaliyohamishiwa maana kutoka lugha ya Kiswahili katika shule ya upili ya Mirangine**

| **Maneno yaliyoandikwa vibaya** | **Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| 'Ona'<br>Umenionea kitabu changu. | *Niunyoneire ibuku riakwa* | Umeshakiona kitabu changu. |
| 'Kata'<br>Nikatie bei ya unga kidogo. | *Ndiniria thogora wa mutu hanini.* | Nipunguzie bei ya unga kidogo |
| 'Mpya'<br>Alipata mtu mpya dukani. | *Akorire mundu mugeni dukaini* | Alimpata mgeni dukani |

Kutokana na makosa waliyofanya ni dhibitisho tosha kuonyesha kuwa wanafunzi wanajaribu kuchukua mpangilio wa maana kutoka lugha yao ya kwanza na kuingiza katika lugha ya pili ambayo ni lugha ya Kiswahili. Makosa mengine waliyoyafanya yalitokana na mwanafunzi kulichukua neno au kifungu cha maneno na kuyapachika katika lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza. Hali hii ilichangia katika kuleta utata katika lugha ya Kiswahili. Hali kadhalika inaonyesha wengine walikuwa wamehifadhi msamiati wa lugha yao ya kwanza walipokuwa wakijifunza lugha ya pili.

### 4.5 Shule ya Upili ya Kangui

Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi katika shule hii ambayo ni ya mseto, mtafiti alipata kuwa msamiati wanaotumia wanafunzi hawa ni mfinyu na umeathirika na lugha yao ya Kikikuyu. Walipatikana wakiwa wamefanya makosa mengi ya kimaana yanayotokana na athari ya lugha yao ya kwanza.

Yafuatayo ni baadhi ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi yanayoonyesha mwingiliano wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 8 Makosa ya kiathari**

| Sentensi zilizoandikwa kimakosa | Tafsiri ya sentensi hizo katika lugha ya Kikikuyu | Kiswahili Sahihi |
|---|---|---|
| Mtu yule 'hutoa' kazi katika idara ya upelelezi wa jinai. | *Mundu uria arutaga wira kwa folithi.* | Mtu yule hufanya kazi katika idara ya upelelezi wa jinai. |
| Mimi ninasikia nikifunzwa na mwalimu yule. | *Nii ni njiguaga ingirutwo ni mwalimu uria.* | Mimi ninaelewa nikifunzwa na mwalimu yule. |
| Mamangu alisaidika vizuri pasipo tatizo. | *Mami niarateithikire hatari thina.* | Mama alijifungua vizuri pasipo tatizo. |
| Hivyo ni kuonyeshana | *Uguo ni kuonania* | Hivyo ni kuonyesha |
| Ameshika alama ya A | *Akinyita 'A'* | Alipata alama ya 'A' |
| Naomba mola anionekanie | *Ngai anyonekanire* | Mungu ajidhihirishe kwangu |
| Mamangu amepewa mtoto | *Maitu akiheo mwana* | Mama alijifungua mtoto |

Haya ni maneno yaliyoandikwa vibaya yanayoonyesha mwingiliano wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 9 Maneno yanayoonyesha kuathiriwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kikikuyu chambilecho uhamishaji na tafsiri sisisi**

| **Maneno yaliyoandikwa vibaya** | **Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Enda: Niendee na kikombe hiki nitakufuata baadaye. | *Thiira na gikombe giki ningukurumirira thutha.* | Enda na kikombe hiki nitakufuata baadaye. |
| Kunywa: Babangu hunywa sigara kila siku jioni. | *Baba nianyuaga thigara hwaini.* | Babangu huvuta sigara kila jioni. |
| Mamangu alichomwa sindano alipokuwa mgonjwa. | *Mami niarathecirwo shindano riria arari muruaru.* | Mamangu alidungwa sindano alipokuwa mgonjwa. |
| Zunguka: Alikuwa akihisi kuzungukiwa alipokuwa mgonjwa | *Araiguaga agithiururukirwo riria arari muruaru.* | Alikuwa akihisi kizunguzungu alipokuwa mgonjwa. |

Wanafunzi walikuwa wakikanganyika walipokutana na neno ambalo lilijitokeza kama homonimu. Kwa mfano neno *'igua'* katika lugha ya Kikikuyu humaanisha kusikia na hali kadhalika kuelewa au kufahamu kitu au jambo Fulani. Kulingana na madai ya Ingram (1994), mwanafunzi anapokutana na neno ambalo linajitokeza kama homonimu huweza kudhania maana ya neno hilo kutokana na maana anayoijua ya neno hilo. Kulingana nadharia ya uchaguzi linganuzi ni kwamba iwapo mwanafunzi anajifunza lugha ya pili ambayo inafanana na lugha ya kwanza huweza kupatikana katika mtego wa maingiliano ya lugha hizi mbili. Kwa hivyo kunatokea hali ya kuathiriana kwa lugha hizi zinazofanana. Kwa sababu lugha ya Kikikuyu na lugha ya Kiswahili ni lugha za familia moja basi hali hii iliweza kutokea sana. Kutokana na sababu hii mwanafunzi aliweza kuelezea maana ya neno kwa kuzingatia mfumo wa lugha yake ya kwanza. Kutokana na hali hii mwanafunzi alihamisha maana kutoka lugha yake ya asili na kuweza kuitumia katika lugha ya pili ambayo alikuwa akijifunza. Kutokana na hayo akaweza kusababisha makosa ya kimaana katika lugha ya Kiswahili ambayo alikuwa akijifunza.

Kwa mfano mwanafunzi aliposema 'mamangu alisaidika vizuri pasipokuwa na tatizo, neno hili kusaidika limetoholewa kutokana na neno la Kikikuyu *'guteithika'* ambalo ni neno la Kikuyu linalomaanisha kujifungua. Hapa ni wazi kusema kwamba mwanafunzi ameathiriwa na lugha ya kwanza anapojifunza lugha ya pili. Inaonekana kuwa mwanafunzi anaeleza maana kutokana na ufahamu alio nao wa lugha yake ya kwanza.

Nadharia hiyo pia inadai kuwa mtoto akiwa mdogo huweza kuhifadhi maneno Fulani katika ubongo wake. Anapokuwa mtu mzima maneno haya huweza kumkanganya na vilevile kumuathiri wakati anajifunza lugha ya pili. Hasa ikiwa lugha hizo zinaonyesha kufanana. Mwanafunzi huyo hujaribu kutumia maneno aliyonayo kujieleza katika lugha ya pili kwa sababu anadhania kuwa lugha hizi mbili zinafanana na mfumo wao ni sawa. Hali hii humletea shida mwanafunzi wakati anajifunza lugha ya pili. Wakati mwanafunzi anapokuwa huweza kutangamana na tajriba mbalimbali na kutokana na tajriba hizo ndipo akaweza kujenga maana ya maneno fulani fulani katika lugha.

Wakati mwingine mwanafunzi aliweza kutafsiri neno moja kwa moja kutoka lugha yake hadi lugha ya pili ambayo alikuwa akijifunza kwa mfano mamangu alipewa mtoto. Sentensi hii inatokana moja kwa moja na ya Kikikuyu *'niaraheirwo mwana'*. Makosa kama haya yaliweza kuwatatiza sana wanafunzi. Mtoto anapokuwa akikua huweza kuona akina mama wakipata watoto na hapo anang'amua kuwa anapewa zawadi ya mtoto. Dhana hii humwathiri anapokuwa na anapojaribu kujieleza. Hali hii inajitokeza kwa sababu utamaduni anaokulia mtoto humwathiri wakati anapojifunza lugha. Kulingana na Mukuthuria (2004), utamaduni unaohitilafiana wa lugha mbili hupelekea mwanafunzi kufanya makosa yanayotokana na lugha mbili kuathiriana.

## 4.6 Shule ya Upili ya Tumaini

Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi katika shule hii, ilijitokeza kwamba hawajaonyesha kuwa na umahiri katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu wameathirika na lugha yao ya Kikikuyu na walionekana wakiweza kuhamisha maumbo na dhana mbalimbali kutoka lugha hiyo hadi lugha ya Kiswahili ambayo walijifunza kama lugha ya pili.

**Yafuatayo ndiyo makosa yaliyopatikana katika shule hii**

Makosa haya yanaonyesha kuwa maana ya maneno imetafsiriwa kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 10 Makosa ya tafsiri sisisi vilevile uhamishaji wa kimaana**

| **Sentensi zilizokuwa na makosa** | **Tafsiri ya sentensi hizo katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Alipatikana akiiba mtihani. | *Aronirwo akiiya kigeranio.* | Alipatikana akidanganya katika mtihani. |
| Alitoa nguo hadharani. | *Ararutire nguo mbere ya andu.* | Alivua nguo hadharani |
| Alishindwa kulipa deni akachotwa. | *Araremirwo ni kuriha thiri aratahwo.* | Alishindwa kulipa deni vitu vyake vikachukuliwa na wadhamini. |

**Maneno yaliyokuwa na makosa**

Makosa yanayotokana na mwingiliano wa kimaana kutoka lugha ya Kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili.

**Jedwali la 11 Leksia za Kiswahili zilizohamishiwa maana kutoka lugha ya Kikikuyu**

| **Maneno ambayo yana makosa** | **Tafsiri ya maneno haya katika lugha ya Kikikuyu** | **Kiswahili Sahihi** |
|---|---|---|
| Chagua: Huu mchele haukuchaguliwa vyema. | *Muchere uyu ndunathurwo wega.* | Huu mchele haukudondolewa vyema. |

Makosa mengi yaliyojitokeza yanaonyesha kuwa mwanafunzi alikuwa akitafsiri maana kutoka lugha yake ya Kikikuyu na kuingiza katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano mwanafunzi anaposema mchele haukuchaguliwa anamaanisha *'thura'* katika lugha ya Kikikuyu. Neno *'thura'* katika lugha ya Kikikuyu humaanisha kuteua na hali kadhalika kudondoa. Basi anapotumia neno hili kuwakilisha tendo la kudondoa mchele huweza kutinga maana katika lugha ya Kiswahili.

## 4.7 Tathmini na Matokeo

### 4.7.1 Tafsiri Sisisi

Baada ya kuangalia makosa yanayofanywa na wanafunzi mtafiti aliweza kuchanganua na kuainisha matapo ya makosa haya. Baadhi ya makosa yaliyotokea ni kama yale yaliyotokana na tafsiri sisisi. Hii ni hali ambapo mwanafunzi huweza kuelezea maana ya neno moja kwa moja kutoka lugha asili hadi lugha ya pili anayojifunza. Wanafunzi hawa waliweza kupatikana na makosa ya maelezo ya lugha ya Kikikuyu moja kwa moja hadi lugha ya Kiswahili. Hali hii huweza kutokea kwa sababu ya mambo kadhaa. Kwa mfano, kulingana na mwanaisimu Butterworth (1983), mwanafunzi huweza kutafsiri maana ya neno anapokosa kirejelewa cha neno ambalo analizungumzia. Anaposhindwa kutafsiri neno hilo kulingana na kanuni za utafsiri basi huweza kulitafsiri moja kwa moja na hapo ndipo utata wa kimaana unaibuka. Wanafunzi walifanya makosa kemkem ya tafsiri sisisi, kwa mfano walikuwa wakiandika "Mamangu alipata mtoto kwa kuchinjwa" kuchinja ni hali ya kuchukua kisu kikubwa na kuanza kukata maungo ya kiumbe chochote chenye uhai kama vile mnyama.

Binadamu anapochinjwa huaga dunia. Mwanafunzi wa Kikikuyu anaposema kuchinjwa kwa mamake anatafsiri neno *'guthinjwo'* kutoka lugha yake ya kwanza yaani Kikuyu ambalo lina maana ya kufanyiwa upasuaji. Na anapofanya hivyo ndipo maana inapotoka na kuweza kutatanisha yule ambaye anayemtahini. Kulingana na maoni ya Catford (1965), mwanafunzi anapotafsiri neno moja kwa moja huweza kupachika maneno mageni kutoka lugha yake ya asili hadi lugha ya pili ambayo anajifunza. Anapofanya hivyo kwa sababu hazingatii kanuni za tafsiri huweza kusababisha makosa ya kimaana. Anaendelea kudai kuwa hali hii hujitokeza wakati mwanafunzi anapokosa kuwa na msamiati wa kutosha katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Mwanafunzi huweza kutafsiri maana ya neno anapojaribu kukopa neno kutoka lugha yake asilia na hapo huweza kusababisha utata wa kimaana. Anafanya hivi anapojaribu kujitanzua kutokana na utata wa kukosa msamiati mwafaka anaotaka kuutumia. Kulingana na maoni ya Lyons (1981), mwanafunzi huweza kutafsiri maana ya neno kwa kuzingatia kinachosheheniwa na neno hilo. Mtoto anapofanya hivyo anaweza kutatiza maana ya neno awali lililokusudiwa na neno hilo na hapo ndipo shida zinapojitokeza.

Makosa haya ya tafsiri ndiyo yaliyoonekana kuwasumbua sana wanafunzi.

- Mtoto yule alipoenda dukani alipata muuzaji mpya kwa hivyo akakataa kununua kile alichokuwa ametumwa, badala ya kusema mtu mgeni.

- Naomba Mola anionekanie – Mola aweze kunisaidia.

- Kikombe kimekufa, badala ya kikombe kimevunjika.
- Alimtia nguo mwanawe, badala ya alivalisha nguo mwanawe.
- Nywele zake zimeiva vizuri, Nywele zimekuwa tayari.
- Alienda hospitalini kutengenezwa kichwa, badala ya kutibiwa kichwa.
- Halima alipiga nguo za mwanawe, badala ya aliosha nguo za mwanawe.
- Mama alisaidika vizuri pasipo tatizo, badala ya kusema mama alijifungua vizuri pasipo tatizo.
- Nasikia njaa, badala ya kusema nahisi njaa.
- Hivyo ni kuonyeshana hakuelewa vizuri badala ya kusema hivyo ni kuonyesha hukuelewa vizuri.
- Kutoa vita badala ya kusema kusababisha vita au vurugu.
- Mama alipata mtoto kwa kuchinjwa.
- Kutoa mavazi ya nyumba badala ya kusema kuondoa mavazi ya nyumba.
- Watu walikula pesa ya serikali, badala ya kusema wanatumia pesa za serikali vibaya.
- Kupea watu heshima, badala ya kupatia watu heshima.
- Serikali haisikii huruma kwa watu, badala ya kusema serikali haiwaonei watu huruma.
- Ameenda kufungwa nywele, badala ya kusukwa nywele.

### 4.7.2 Makosa yanayotokana na Uhamishaji wa Maana

Haya ni makosa yanayotokana na mwanafunzi kuhamisha dhana na vipengele mbalimbali vya kimaana kutoka lugha yake ya Kikikuyu na kuingiza katika lugha ya Kiswahili. Makosa haya yalionyesha jinsi wanafunzi walivyoathiriwa na lugha ya Kikuyu wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Crowly (1982), anadai kuwa kuna misukumo kadhaa ambayo inawafanya watu na hasa wanafunzi kuhamisha maana ya neno kutoka lugha moja hadi nyingine, hasa kutoka lugha asilia hadi lugha ya pili ambayo mwanafunzi anajifunza.

Kwanza kabisa mwanafunzi huhamisha maana ya neno kutoka lugha ya kwanza hadi lugha anayojifunza kwa sababu ya hali inayojulikana kama upanuzi wa kimaana. Hali hii huweza kutokea ikiwa mwanafunzi amelemewa na msamiati wa neno katika lugha ya pili. Kwa hivyo kile anachojaribu kufanya ni kuupanua msamiati wa neno alilo nalo ili kukabiliana na hali inayomtatiza. Kwa mfano anaposema Mola anionekanie anajaribu kunyambua neno alilonalo

kwenye mawazo yake ya lugha asilia na kuweza kukidhi mahitaji aliyonayo. Neno hili limetoholewa kutoka lugha ya Kikikuyu *'anyonekanire'* yaani Mungu ajidhihirishe kwangu. Jambo jingine ambalo linafanya wanafunzi kuhamisha maana ni hali ambayo inajulikana kama ufinyanzi wa maana ya neno. Mwanafunzi anapolemewa na msamiati wa kutosha huweza kufinyanga neno hilo na kuweza kuwa na maana nyingine tofauti kabisa. Kwa mfano neno kama vile kufinyilia mtu linatokana na neno *'kuhinyiriria'* katika lugha ya Kikikuyu.

Wakati mwingine mwanafunzi huweza kuandika neno hilo. Hali hii huweza kutokea kwa sababu ya mwingiliano wa kimaana kutoka lugha zinazokaribiana kama vile Kikuyu na Kiswahili. Wanafunzi hukopa msamiati kutoka lugha zao asilia wanapojaribu kuelewa lugha na tamaduni za lugha anayojifunza. Kwa mfano neno unda katika lugha ya Kikikuyu humaanisha kutengeneza kitu na hali kadhalika mwanafunzi kutoka jamii hii anaweza kusema kuunda nyumba. Mwanafunzi anapojaribu kuelewa lugha ya Kiswahili na tamaduni zake hujipata amehamisha maana kutoka lugha ya Kikikuyu na hapo anasababisha makosa ya kimaana kwa mfano ni makosa kusema kuunda nyumba kumaanisha kujenga nyumba katika Kiswahili sanifu. Hali hii huweza kutokea kulingana na nadharia ya uchanganuzi linganuzi ambayo inadai kuwa mwanafunzi huweza kutatizika anapojaribu kuelewa tamaduni ya lugha ya pili anayojifunza na hapo ndipo utata wa kimaana unapojitokeza.

Mwanafunzi alionekana akihamisha maana kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ambayo alikuwa akijifunza. Hii ni kwa sababu tayari mwanafunzi kama huyu huwa amehifadhi msamiati wa lugha yake katika leksikografia ya ubongo wake na anajaribu kuelezea maana ya neno kutokana na ufahamu alionao wa lugha yake ya asili katika ufahamu wa ubongo wake. Mtafiti aligundua kuwa wakati mwanafunzi anatatizika na maana ya neno geni katika lugha anayojifunza hapo ndipo huweza kuhamisha maana ya neno alilo nalo katika ubongo wake na kuweza kulieleza katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Yafuatayo ndiyo baadhi ya maneno ambayo yamehamishwa. Kuonyesha kuwa mwanafunzi hakuwa na uchaguzi wa neno mwafaka katika leksia inayowakilisha dhana mbalimbali katika ufahamu wa ubongo wake. Kama maneno yamefanana mwanafunzi huchanganyikiwa.

Maneno ambayo yalihamishwa maana na wanafunzi kutoka jamii ya Kikikuyu hadi Kiswahili.

- Wewe ndiwe ulituma nichelewe badala ya kusema wewe ndiwe ulifanya au ulisababisha nikachelewa.
- Baba yule ameunda nyumba badala ya kusema amejenga nyumba.

- Mtoto yule alimtupa mtoto mwenzake akapepesuka na kuanguka badala ya kusema alimsukuma mwenzake akaanguka.
- Nikatie pesa badala ya kusema nipunguzie bei.
- Ninapiga nguo badala ya kuosha nguo.
- Kutoa nguo hadharani badala ya kuvua nguo hadharani.
- Ninasikia njaa badala ya kusema ninahisi au naona njaa.
- Mamangu alipewa mtoto badala ya kuandika mamangu alijifungua mtoto.
- Alipatikana akiiba mtihani badala ya kusema kudanganya katika mtihani.
- Kukomboa nyumba badala ya kupanga nyumba.

Ile dhana ambayo imewakilishwa katika ubongo wa binadamu kuhusu leksia Fulani ndiyo inamkanganya mwanafunzi na kusababisha afanye makosa. Ikiwa maneno yanakaribiana mwanafunzi hutatanika katika uchaguzi wa neno mwafaka kwa sababu vipengele hivi vya kimaana vimepangwa karibu karibu katika ubongo wa mwanafunzi.

### 4.7.3 Ubadilishanaji wa Maneno

Hii ni hali ambayo inatokea wakati mwanafunzi hupachika neno kutoka lugha yake katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Hii ni kwa sababu maana ya maneno haya ya lugha ya pili hayajaratibiwa vizuri katika leksikografia ya mwanafunzi anayejifunza lugha ya pili. Ule msamiati alio nao unamkanganya na anautumia vibaya anapojaribu kujielezea katika lugha hii ya pili anayojifunza. Wanafunzi hubadilisha maneno kwa sababu ya hali ya maneno haya kufanana. Kwa mfano mama amekomboa nyumba katika mtaa ule. Neno komboa linatokana na neno la Kikikuyu '*Gukombora*' ambalo lina maana ya kupanga kwa hivyo mwanafunzi huweza kubadilisha maana ya neno hilo na kuweza kulipachika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Hali hii inapotokea kunatokea athari za kimaana kwa sababu neno linabadilisha maana inayokusudiwa. Neno tupa katika lugha ya Kikikuyu huwakilisha hali ya kurusha kitu na hali kadhalika kusukuma. Kwa hivyo kwa sababu ya kufanana kimaana mwanafunzi anapokumbana na neno hili katika lugha ya Kiswahili huweza kufikiria maana inamaanisha sawia katika lugha ya Kiswahili na hali hii huweza kumletea matatizo ya kimaana. Kauli hii inaungwa mkono na Garman (1994).

Iligunduliwa kuwa maneno ambayo ni homonimu au sinonimia yaliweza kubadilishwa na mwanafunzi hata bila mwanafunzi kugundua kuwa amefanya makosa. Hii ni kwa sababu

maneno ambayo yanakaribiana huweza kuwasilishwa au kuwekwa pamoja katika ubongo wa binadamu na mwanafunzi huweza kutumia maneno haya pasipo kung'amua kama amesababisha makosa. Kwa mfano neno tuma katika lugha ya Kikikuyu huweza kumaaanisha kusababisha na hali kadhalika kumuuliza mtu aende mahali Fulani akatekeleze wajibu Fulani. Mwanafunzi wa Jamii ya Kikuyu alikuwa haoni shida yeyote kusema wewe ndiwe ulituma nikachelewa lakini twajua haya ni makosa katika lugha ya Kiswahili sanifu.

Vilevile mwanafunzi aliweza kubadilisha neno ili kuepukana na shida inayomkabili na hali hii humfanya aidha kufinyanga neno linalomsumbua au kutumia mbinu zake maalum kuunda neno litakalofaa katika hali yake. Kwa mfano baadhi ya wanafunzi walikuwa wakiandika neno 'kusondeka' kuwakilisha kutengeneza kitu. Neno hili ni la lugha ya Kikikuyu linalotamkwa *'guthondeka'* yaani kutengeneza. Iwapo mwanafunzi amepatikana na hali ngumu kama ya kukosa msamiati wa kutosha huweza kuliunda neno kama hili ili kukidhi mahitaji yake na hapo makosa haya yanajitokeza. Mwanafunzi anaandika neno linalokaribia msamiati alio nao katika lugha yake ya kwanza.

Makosa haya yanayofanywa na mwanafunzi yanadhihirisha hali yake ya Leksia katika ubongo wake. Iwapo ameathirika sana na lugha yake ya kwanza ndipo tunamwona akisababisha makosa mengi yanayotokana na lugha yake ya kwanza. Maoni haya yameungwa mkono na Garman (1996). Anaendelea kusema kuwa mwanafunzi husababisha makosa ya ubadilishanaji anapojaribu kuiwakilisha lugha yake katika lugha ya pili ambayo anajifunza. Haya ni makosa yaliyotokana na ubadilishanaji wa maneno.

- Kushika samaki badala ya kuvua samaki.
- Ambia Mary aje ajioge badala ya ambia Mary aje aoge.
- Kenya na Uganda walichapana badala ya walipigana.
- Nimeinamilia pale hadi nikakuona badala ya nimeinama pale hadi nikakuona.
- Nilikuwa nikienda akanitupa badala ya nilikuwa nikienda akanisukuma.
- Mama ameenda kufungwa nywele badala ya kusukwa nywele.
- Kusondeka badala ya kutengeneza
- Alishindwa kulipa deni akachotwa.

### 4.8 Umaratokezi wa makosa haya

Baada ya kuangalia sababu za kuwepo kwa makosa haya mtafiti aliona ni mufti kuangalia athari ya makosa haya kwa wanafunzi hawa wazawa wa lugha ya Kikikuyu. Makosa haya

yalichanganuliwa kwa kuangalia umaratokezi wake kisha kutathmini asilimia ya makosa haya.

Makosa haya yaliweza kutathminiwa kwa kutumia kielelezo hiki $\frac{X}{Y} \times 100$

Alama X inasimamia aina ya makosa.

Alama ya Y inawakilisha jumla ya wanafunzi waliofanyiwa utafiti.

Makosa yaliwekwa katika jedwali ambalo linaonyesha makosa haya yalivyojitokeza mara ngapi katika kila shule.

**Jedwali la 12 Asilimia ya makosa ya tafsiri sisisi**

Idadi ya wanafunzi waliofanya makosa haya

| Shule ya Nyakiambi | Tumaini | Mirangine | Sabugo | Kangui |
|---|---|---|---|---|
| 6 | 11 | 12 | 10 | 7 |

Asilimia = $\frac{46}{100} \times 100 = 46\%$

**Jedwali la 13 Asilimia ya makosa ya uhamishaji**

| Shule ya Nyakiambi | Tumaini | Mirangine | Sabugo | Kangui |
|---|---|---|---|---|
| 8 | 10 | 11 | 12 | 9 |

Asilimia = $\frac{50}{100} \times 100 = 50\%$


**Jedwali la 14 Asilimia ya makosa ya ubadilishanaji**

| Shule ya Nyakiambi | Tumaini | Mirangine | Sabugo | Kangui |
|---|---|---|---|---|
| 7 | 11 | 10 | 10 | 7 |

Asilimia = $\frac{45}{100} \times 100 = 45\%$

Makosa haya yaliweza kuwakilishwa katika grafu kwenye mihimili.

**Jedwali la 15 Tathmini ya jedwali la asilimia moja ya makosa**




Grafu hii inaonyesha matapo mbalimbali ya makosa yaliyofanywa na wanafunzi. Hali hii ina maana kuwa wanafunzi hufanya makosa yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Hali hii inawafanya wanafunzi kutofanya vyema katika lugha ya Kiswahili hasa katika karatasi ya insha kwa sababu katika mtihani wa insha wanafunzi hulazimika kujieleza kimaandishi. Baadhi ya shule hazina makosa mengi kama zile zingine kwa sababu zingine ni za bweni kwa hivyo wanafunzi wanatangamana na wanafunzi kutoka sehemu zingine ambao hawana athari hiyo ya lugha ya Kikikuyu.

Makosa haya yaliwekwa katika viwango tofauti ili kuchanganuliwa vyema.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kiwango cha arobaine kwa mia | = | mwanafunzi ameathirika kwa wastani. |
| 2. | Kiwango cha hamsini na kuendelea | = | mwanafunzi ameathirika sana. |

Makosa haya ndiyo yaliyojitokeza kuwalemea sana wanafunzi kwa sababu ya athari ya lugha ya kwanza.

Baadhi ya makosa haya ni yale yanayotokana na uhamishaji. Wanafunzi walikuwa wakihamisha dhana kutoka lugha yao ya Kikikuyu na kuyaingiza katika lugha ya Kiswahili waliyokuwa wakijifunza kama lugha ya pili. Kwa mfano neno unda katika lugha ya Kikikuyu huwa na maana ya *'tura'* kama vile mhunzi anavyoweza kuunda vitu vya chuma katika maumbo tofauti totauti au kama mfinyanzi anavyofinyanga vitu vya udongo katika sura mbalimbali kutokana na

maana hii walifikiria wanaweza kutumia neno hili katika lugha ya Kiswahili kumaanisha kujenga. Mfano, walikuwa wakisema aliunda nyumba nzuri. Hali hii iliweza kuleta utata katika lugha ya Kiswahili.

1. Makosa mengine yaliyotokana na ubalishanaji na mengine yanatokana na udhanifu na hali kadhalika uteuzi mbaya wa msamiati katika sentensi zao.

## 4.9 Chanzo cha Makosa

Ili kuweza kulijibu swali hili vyema ni murua kufahamu kuwa kadri lugha zilivyo tofauti ndivyo miundo na mitindo yake ilivyo tofauti. Hata ingawa lugha zinaelekea kufanana lazima kuwepo na utofauti katika viwango mbalimbali vya lugha hizi. Hii ndiyo hali ambayo Kiswahili na Kikikuyu hujipata. Lugha hizi mbili ni za kibantu na ingawa zinafanana kimaongezi kwa kiwango fulani miundo yake hata ya kimaana ni tofauti kabisa. Baadhi ya sababu hizi huchangia kuwepo kwa makosa katika lugha ya Kiswahili.

### 4.9.1 Mfumo wa ngeli katika lugha ya Kiswahili

Wanafunzi wa jamii ya Wakikuyu hufanya makosa ya kimaana kwa sababu wanashindwa kuainisha maneno vizuri kulingana na ngeli za majina ya Kiswahili. Wanashindwa kuelewa kuwa ili maana ijitokeze barabara lazima wazingatie ukubaliano wa kisarufi na maana kwa mantiki ili kusitokee utata wowote katika kujieleza kwao. Ili wasitatizike ni lazima basi waelewe vyema mfuatano wa ngeli na majina yote yanayopatikana katika lugha ya Kiswahili. Kiswahili kina takriban ngeli au makundi kumi na sita ya majina. Makundi haya yamepangika katika makundi mawili, la umoja na lingine la wingi. Mathalan mtu (umoja) watu (wingi). Majina katika lugha ya Kiswahili ni muhimu sana. Katika Kiswahili sanifu inambidi mzungumzaji kupatanisha nomino au jina na maneno ya sifa kama vile – zuri – baya.

Almuradi sentensi katika Kiswahili sanifu haiwi imara kisarufi ikiwa nomino haikupatanishwa kwa njia inayokubalika na maneno mengine katika sentensi. Haya ni madai ya King'ei (2002). Kwa mfano:

| **Kiashiria** | **Jina** | **Kimilikishi** | **Kitenzi** |
|---|---|---|---|
| Kile | Kiti | Changu | Kimevunjika |

Katika sentensi hii jina kiti limepatanishwa vizuri na maneno mengine katika sentensi. Neno **ki** limeacha athari zilizo bayana kwenye maneno mengine katika sentensi. Hii ina maanisha kuwa jina au nomino ya Kiswahili sanifu haina budi kuonyesha athari yake katika majina

mengine katika sentensi. Wanafunzi wengi hupuuza upatanisho huu na ndiposa makosa ya sarufi na kimaana yanapotokeza. Baadhi yao huona shida wanapojaribu kufuata kanuni hizi za upatanisho wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walioathiriwa sana ni wale ambao wanatoka katika jamii ya Kikuyu wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Hii ni kwa sababu lugha ya Kikikuyu huwa na shida za mpangilio wa ngeli katika mfumo wake. Ngeli katika lugha hii hazijaainishwa vyema kama vile lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu utaweza kupata majina mengine ya binadamu yametapakaa katika ngeli zingine. Kikikuyu kimeorodheshwa kuwa na makundi 14 ya ngeli kulingana na jarida liloandikwa kwa heshima ya Guthrie (1970). Jedwali hili linadai kuwa mpangilio wa majina haya hauko vyema. Hii ndiyo sababu ambayo inawasumbua wanafunzi hawa wanapokuwa wakitunga sentensi ambazo lazima zionyeshe ukubaliano wa majina katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi wa lugha ya Kikikuyu hujaribu kuyaweka majina au nomino Fulani katika ngeli zisizofaa. Kwa mfano majina mengine huingia katika ngeli ya **(ma)** na hayawezi kuingizwa katika ngeli ya **(ji).** Wanafunzi walikuwa wakiandika sentensi kama hizi.

**Mfano:**

- Hitaji langu ni kazi nzuri. (ngeli ya ma)
- Ningependa kutoa oni langu.

  Sentensi sahihi ni
- Mahitaji yangu ni kazi nzuri. (ngeli ya ji).
- Ningependa kutoa maoni yangu.

### 4.9.2 Unyambuaji wa Maneno

Lugha zote za Kibantu huwa na unyambuaji wa maneno katika vipengele mbalimbali. Kuna mnyambuliko wa vitenzi katika lugha ya Kiswahili na hali kadhalika Kikikuyu. Iligunduliwa kuwa mwanafunzi wa jamii ya Kikuyu hutumia muundo wa lugha yake katika unyambuaji wa maneno na hali hii huweza kumletea matatizo. Hasa kwa upande wa maana. Kwa mfano wanafunzi walikuwa wakiandika serikali 'inafinyilia' watu wake. Kitenzi hiki hutokana na kitenzi cha Kikikuyu *'kuhinyiriria'* ambapo katika lugha ya Kikikuyu husimamia neno kugandamiza. Mwanafunzi anapolinyambua au kuliandika neno namna hii huwa anasababisha makosa ya kimaana. Kulingana na Dordretch (1987), upekee unaopatikana katika miundo mbalimbali ya lugha unatokana na tofauti za leksia kati ya lugha mbalimbali na jinsi sheria za ugeuzi zinavyofanya kazi ili kuwa na umbo nje na umbo ndani.

Hivi ni kumaanisha kuwa ugeukaji wa maneno katika lugha moja huwa tofauti na lugha nyingine na mwanafunzi anapojaribu kutumia muundo wake kuelewa lugha ya pili hujipata matatani na huweza kuchanganyikiwa na kupotosha maana. Kwa mfano lugha ya Kikikuyu inaweza kuwa na mfano wa mpangilio wa maneno kama haya katika sentensi bila kusababisha utata.

*Rehema niaranengerire Roda karamu.*

*Rehema niaranengeranire karamu kwi Roda.*

*Rehema niaranengeraniire karamu kwi Roda.*

Katika lugha ya Kiswahili tunaweza sema:

Rehema alimpatia Roda kalamu.

Rehema alipatiana kalamu kwa Roda

Hali hii ina maana kuwa lugha ya Kikikuyu hukubalia usogezi wa vipengele mbalimbali katika sentensi bila kufuata sheria yeyote maalum lakini mwanafunzi wa lugha ya Kiswahili akijaribu kufanya hivyo huweza kusababisha utata wa kimaana. Maw (1969) anaunga mkono kauli hii.

### 4.9.3 Uteuzi wa msamiati usiofaa

Mara nyingi wazungumzaji wengi hasa wanaoathiriwa na lugha ya Kwanza hutumia maneno yasiyofaa katika muktadha mbalimbali ukiwemo muktadha wa darasani. Matokeo ya matumizi kama haya ni sentensi iliyo sahihi kisarufi lakini iliyo na kasoro ya kimaana. Wanafunzi wa jamii ya Kikuyu kwa kuwa wameathiriwa na shida kama hii walipatikana na makosa kama vile:

- Nilienda dukani nikapata mtu mpya, sentensi kama hii ina makosa. Hatuwezi kuwa na mtu mpya kama vile nguo au kitu bali tunaweza kuwa na mtu mgeni.
- Yeye hutoa kazi kwa polisi. Sentensi sahihi ni yeye hufanya kazi kwa polisi.

### 4.9.4 Marudio katika lugha ya Kikikuyu

Lugha ya Kikikuyu ina marudio mengi ya maneno yaliyo na dhana yenye maana sawa. Hali hii huweza kumtatiza mzungumzaji au mwanafunzi anayejifunza lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, tazama sentensi kama hii:

- *Ngwenda ati undeithie.*
- *Ndarumia ati undeithie.*
- *Ndirenda ati undeithie.*

Maneno haya *'ndarumia,' 'ndirenda,' 'ngwenda'* humaanisha kitu kimoja yaani nataka. Hali hii ya kuwa na maneno yanayorudiwa rudiwa hufanya wanafunzi wa jamii ya Kikuyu hata kuwa na makosa mengi ya kimaana na mengine ya mianzo mibaya. Kwa mfano wanafunzi wengine walikuwa wakiandika Ninaanzia na kusema kuwa halafu wanaendelea na sentensi kama hii. Huu ni mfano wa mwanzo mbaya wa sentensi na vilevile unaoleta utata wa kimaana.

## SURA YA TANO

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Katika sura hii hoja mbalimbali zimejadiliwa ambazo zimetoa mapendekezo yatakayotoa suluhisho zitakazosaidia kutatua baadhi ya shida zinazokumba wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Kikikuyu kama lugha ya kwanza wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Mtafiti ameweza kutoa hitimisho zilizounga mkono nadharia tete za utafiti wake.

### 5.2 Hitimisho

Kulingana na matokeo ya utafiti inadhihirika kuwa wanafunzi wazawa wa lugha ya Kikikuyu hufanya makosa mengi yanayotokana na athari ya lugha ya kwanza. Makosa haya aghalabu husababisha kutofanya vizuri katika mitihani yao hasa mtihani ule wa insha kwa sababu unahusu kujieleza kimandishi. Pia makosa haya yanaathiri umahiri wao wa lugha ya Kiswahili hasa wanapokuwa wakiwasiliana.

Kutokana na hali hii suluhisho lapaswa kufikiwa ili kujaribu kutatua baadhi ya shida hizi zinazowakabili. Kwa mfano, mikakati ifaayo yapaswa kushirikishwa ili kujaribu kuwasaidia wanafunzi kama hawa wa jamii ya Kikuyu. Utafiti huu uliweza kuthibitisha nadharia tete ambazo zilidai kuwa wanafunzi hawa huwa na makosa chungu nzima yanayowafanya kutatiza maana katika lugha ya Kiswahili na kwa kiwango kikubwa wameathirika kutokana na lugha hii yao ya kwanza.

### 5.3 Mapendekezo

1. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha kuwa wanafunzi walikuwa na makosa mengi ya kiathari. Baadhi ya makosa waliyofanya yalitokana na kutofahamu vyema muainisho wa nomino za ngeli katika lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu ngeli za nomino za lugha ya Kiswahili hazijaainishwa vyema. Haileweki ni sheria zipi zinatumika kugawa nomino za ngeli katika makundi mbalimbali. Hali hii huwatatiza sana wanafunzi wanapojifunza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili haswa wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu. Kwa sababu Kikuyu ni lugha ya Kibantu. Jambo hili linawafanya wanafunzi kuchanganya nomino katika makundi yasiyofaa. Hali hii huwafanya wanafunzi kutunga sentensi zisizokubalika kwani fahiwa itakuwa imehasirika na kupotoka. Kutokana na hali hii napendezeka ngeli hizi ziweze

kukarabatiwa upya huku sheria zinazotumika kugawa makundi haya ya nomino zikiweza kuelezewa wazi. Hali hii itasaidia wanafunzi kuweza kufahamu dhana ya ngeli pasipo kukariri kariri nomino katika makundi haya.

Hii itasaidia sio tu wanafunzi, mbali itachangia katika kuhamasisha wanaisimu na wataalam wa lugha ya Kiswahili jinsi ya kutatua swala hili nyeti la ngeli za nomino katika lugha ya Kiswahili.

2. Kwa kuwa wanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu wameathirika sana na lugha yao ya kwanza wanapojifunza Kiswahili, napendekeza kuwa mwalimu akiwa darasani awe tu mwelekezi bali muda mwingi upewe wanafunzi ili waweze kujijulia maarifa mengine wao wenyewe. Hali hii itawasaidia kupanua hali ya uasilia ambayo binadamu amezaliwa nayo na angalau iweze kumsaidia kukabiliana na tatizo hili la athari ya lugha ya kwanza wanapofunzwa lugha ya pili. Hali hii itamwelekeza mwanafunzi kufanya mazoezi mengi ya lugha yeye mwenyewe. Jambo hili litamfaa zaidi mwanafunzi. Mfumo wa elimu nchini Kenya hasa katika shule za upili unaegemea kwa upande wa mwalimu. Mwalimu ndiye anayemiliki masomo darasani. Wanafunzi huchangia mada kwa nadra sana. Wao ni wasikilizaji tu. Hali hii hudhuru sana somo la lugha. Kwa vile wanafunzi hawana nafasi ya kutosha ya kujielezea kimaongezi jambo ambalo ni muhimu katika ufunzaji wa lugha.

3. Utafiti huu uligundua kuwa lugha ya Kikuyu ina marudio mengi ya maana ya neno moja. Hali hii huweza kuwatatiza sana wanafunzi wa jamii ya Kikuyu wanapojielezea katika lugha ya Kiswahili. Wanashindwa kubainisha neno litakalofaa katika matini fulani. Kutokana na haya napendekeza mafunzo zaidi kuhusiana na msamiati yaweze kuzingatiwa katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili.Hii itawasaidia wanafunzi kuwa na msamiati wa kutosha na kirejelewa kifaacho cha neno hilo katika lugha ya Kiswahili wanapojielezea. Somo hili kuhusu msamiati wa lugha limeanza kupuuziliwa mbali katika mfumo wa elimu wa 8-4-4 hapa nchini. Jambo hili litakuwa tisho katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili hasa wanafunzi katika jamii ya Kikuyu.

4. Matokeo ya utafiti huu yameonyesha jinsi mwanafunzi kutoka jamii ya Kikuyu alivyoathiriwa na lugha ya kwanza anapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili. Napendekeza waalimu na wataalam mbalimbali wa lugha waweze kuvutwa nadhari kuhusiana na jambo

hili ili waweze kuzua mbinu na mikakati ya kuwasaidia wanafunzi hawa wanapotangamana nao. Kwa mfano kuna hali ya asili kuhusu lugha ambayo binadamu amezaliwa nayo na inaweza kupanuliwa ili kuwasaidia wanafunzi kama hawa. Hii inaweza fanywa kwa kukariri kariri maneno na vifungu vya kinadhari vinavyowaletea shida wanafunzi. Pia kwa kurudia rudia maneno na kuwashauri zaidi wanafunzi.

5. Iligunduliwa kuwa wanafunzi walionekana wakiwa na tatizo la mnyambuliko wa vitenzi. Walikuwa wakitumia kauli za lugha ya Kikikuyu kunyambua maneno katika lugha ya Kiswahili. Jambo hili lilihasiri maana ya neno lililonyambuliwa na mwanafunzi. Kutokana na hali hii napendekeza masomo na ushauri zaidi ufaao ufanyiwe wanafunzi hawa kuhusiana na tatizo hili.

Fauka ya hayo ilibainika kuwa wanafunzi wa kike walionekana wakimudu lugha kuliko wenzao wa kiume. Hii ni kutokana na alama za juu walizozipata dhidi ya wavulana data ilipochanganuliwa na hata ufasaha wao wa lugha. Kwa hivyo napendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusiana na swala hili, katika somo la Isimu jamii linalojishughulisha na lugha na uana. Isitoshe, napendekeza utafiti zaidi ufanywe kuhusiana na jinsi binadamu anavyoweza kupanua data ya kimaumbile au hali uasilia ambayo amezaliwa nayo ya jinsi itakavyomsaidia kukabiliana na matatizo ya kiathari anapojifunza lugha ya pili.

## MAREJELEO


Allwright M. and Bailey K. (1991) *Focus on the Language Classroom.* Cambridge. Cambridge University Press.

Alwright D. (1989) *Observation in the Language Classroom.* Longman Group U.K. Ltd.

Atkins G. (1970) *African Language Studies.* London Luzac &Company Ltd.

Bleek W. (1862) *Comparative Grammar Of South African Languages. Trubner and Co. London.*

Bryman A. (1994) *Quantitative Data Analysis for Social Scientists.* London. Oxford University Press.

Butterworth A. (1983) *Language Production ,Development and Other Language processes.* New York. Academic Press Inc.

Catford J. (1965) *Linguistic Theory of Translation.* Oxford. Oxford University Press.

Chomsky N. & Halle B (1970) *Sound Patterns of English.* New York.Harper and Row publishers.

Chomsky N.(1981) *Language and mind.* NewYork. Harcourt Brace.

Corder S.P.(1981) *Error Analysis and Interlanguage.* Oxford. Oxford University Press.

Cresswell M.J. (1984) *Language in the world.* Cambridge. Cambridge University press.

Crowley T. (1982) A*n introduction to Historical linguistics.* Oxford. Oxford University Press

Cruse D.A (1986) *Lexical Semantics.* Cambridge. Cambridge University press

Dixon R.M.W. *(1992) A New Approach to English Grammar on Semantic Principles.* Cambridge University Press.

___________ (2004) East African Standard Nairobi.

Dordrecht W.(1987)*Word order and word order change.* Austin. University of Texas press.

Dressler W.U (1988) *"Language Death."* In. *Linguistics.* The Cambridge survey IV Newmeyer, F.J(ed); Cambridge. Cambridge University Press.

Dromi E. (1987) *Early Lexical Development.* Cambridge University Press.

Everson J. (1994) *Language.* Cambridge. Cambridge University Press.

Ferguson M. (1989) *Language Structure and Language Use.* California. Stanford University press.

Garman M.(1994) *Psycholinguistics.* Cambridge. Cambridge University Press.

Garman M. (1996) *Language Acquisition.* Cambridge. Cambridge University Press.

Gold Smith B.and Huck G. (1995) *Ideology and Linguistic Theory.* London & New York. Published by Routedge.

Guthrie M. (1970) *The Classification of the Bantu Languages.* London. Oxford University Press.

Halliday M.A.K. (1975) *Learning How to Mean.* Edward Anorld Publishers Ltd.

Hearsley B.&Hurford J. (1993) *Semantics Course Book.* Cambridge. Cambridge University Press.

Hooper J. & Fraugott E. (1993) *Grammatization.* Cambridge. Cambridge University Press.

Ingram (1994) *First Language Acquisition.* Cambridge. Cambridge University Press.

Janda I. and Brian M.(2003) *Historical linguistics.* London. Blackwell Publishing Ltd.

Johnson K. (1747) *"A Century of Bantu Lexicography."* In. African language studies Vol.V School of Oriental and African Studies. London. University of London.

Kariuki M. (2000) *Aspects of Syntactic Information Packaging.* Ph.D. Thesis Egerton University.

King'ei N. na Musau K.(2002) *Utata wa Kiswahili Sanifu.* Nairobi. Sunlitho Limited.

Klein W. (1986) *SecondLlanguage Acquisition.* Cambridge. Cambridge University Press.

KNEC (1997) 1995 KCSE Examination report. Nairobi.

Kothari C.R (2002) *Research Methodology.* Methods & Techniques New age International Limited New Delhi.

Komunte B.S (2001) "The *Impact of Bantu Languages in the English Language Learning process in Tanzanian Secondary Schools."* In. *Makala ya Kongamano la Kimataifa.* Kiswahili *2000* J.S Mdee na H.J.M Mwansoko (Wahariri) Tuki. Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Lado R. (1957) *Linguistics Across Cultures.* Michigan. University of Michigan Press.

Lass R. (1991) *An Introduction to Basic Concepts.* Cambridge. Cambridge University Press.

Lyon J. (1981) *Language and Linguistics.* Cambridge. Cambridge University Press.

Maw J. (1969) *Sentences in Swahili.* London. Luzac & Company Ltd.

Mochiwa Z. (1979) "*The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages.* A Case Study from Handeni Distrct "[Unpublished] M.A Thesis.University of Dar-er-Salaam.

Mosha, M. (1971) *"Loan Words in Luganda; A Search for Guides in the Adaptation of African Languages to Modern Conditions."* In. Whiteley, W. H. (ed) *Language Use and Social Change;* O.U.P., International African Institute London, (pp 228-307)

Mukuthuria M. (2004) *Kuathiriana Kwa Kiswahili na Kimeru.* Tasnifu ya uzamifu. Chuo Kikuu cha Egerton.

Mulliga n K. (1990), *Mind, Meaning and Metaphysics*. London. Kluwer Academic Publishers.

Newmeyer F.J (1993). *Grammatical Theory, its Limits and its Possibilities.* Chicago. University of Chicago press.

Nurse, D (1980) *Bantu Migration into East Africa. Alinguistic Evidence "Paper No 138.* [Unpublished] Institute of Africa Studies (IAS), University of Nairobi.

Odlin, T. (1994) *Cross-Linguistic Influence in Language Learning*. Cambridge. University Press.

Postman, N. (1996) *Linguistic. New York* Manufactured In U S A.

Radford A. (1992*), Transformational Grammer.* Cambridge. Cambridge University Press.

Ravin Yael. (1990) *Lexical Semantics Without Thematic Roles*. Oxford University Press

Rubanza Y.I.(1979) *The Relationship Between Kiswahili and Other African Languages*. The Case Study of Kihanya. [Unpublished M.A Thesis] University of Dar er Salaam.

Schmidt.R (1988)*The Potential of PDP for SLA theory and research.* In. UHWPESI.

Schlesinger M. (1982) *Cognitive structures and semantic structures.* Cambridge. Cambridge University Press.

Seliger H &Schohanmy E. (1990) *Second Language Reseach Methods*. New York. Oxford University Press.

Selinker, L. (1972) *Rediscovering Interlanguage*. New York. Longman Group USA.

Thomas J. (1995) *Meaning in Interaction*. London. Longman Group Ltd.

Wallwork J.F. (1985) *Language and Linguistic*. London. Heinemann Education Books

Weinreich P. (1968) *Language in Contact*. Mouton the Hague London. Trubner And Co.

Were-Mwaro, A.G (2000) *"Usayansi wa Istihali za Isimu ya Kiswahili."* Tasnifu Ya Uzamifu [Isiyochapishwa] Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

## Kiambatisho A

Katika mkabala huu, wanafunzi waliulizwa kuandika insha kuhusiana na mada hizi. Mada hizi ziliteuliwa kwa sababu ni mada shawishi. Ziliwachochea na kuwashawishi wanafunzi kujielezea kwa kina. Kutokana na haya makosa mengi ya kisemantiki yaliweza kujitokeza. Isitoshe, mada hizi zina sampuli ya masuala ibuka. Haya ni masuala yanayochipuka nchini na hata ulimwenguni. Wanafunzi huulizwa kuandika insha za aina hii shuleni, na hata katika mtihani wa mwisho wa kidato cha nne. Kwa kawaida wanafunzi huagizwa kutumia idadi fulani ya maneno isiyo chini ya kiwango cha mia tatu.

Andika insha zifuatazo kwa kutumia maneno yasiyozidi wala kupungua mia tatu kwa kufuata maagizo uliyopewa.

1. Andika insha kuhusu hatua ambazo serikali yapaswa kuchukua kufufua uchumi wa nchi hii.

2. Andika insha inayohusu methali hii: Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

3. Andika insha kuhusu hotuba hii: Umealikwa kama mgeni mheshimiwa katika kata yako, toa hotuba kuhusu jinsi ya kuimarisha usalama wa wananchi wa kata hii.

## Kiambatisho B

Katika mkabala huu wanafunzi walipewa maneno kisha wakaulizwa kuyatungia sentensi. Maneno haya yamebeba leksia za Kikikuyu. Mtafili aliposahihisha sentensi hizi aliangalia iwapo mwanafunzi atapotoka na kuhamisha maana iliyoko ya lugha ya Kikikuyu kutoka leksia hizi katika lugha ya Kiswahili.

**4. Tunga sentensi ukitumia maneno uliyopewa huku ukionyesha maana ya maneno haya.**

(a) Tupa
(b) Tuma
(c) Enda
(d) Sikia
(e) Unda
(f) Shika
(g) Kata
(h) Osha
(i) Pita
(j) Pika

**(ii) Sentensi hizi zina makosa gani?**

Sentensi hzi zinadhihirisha maana ya moja kwa moja kutoka lugha ya Kikikuyu. Kwa mfano kutengenezwa kichwa kwa maana ya 'Guthondekwo mutwe' katika lugha ya Kikikuyu. Kwa hivyo sentensi hii ina makosa ya kimaana iliyohamishiwa lugha ya Kiswahili. Mtafiti alitarajia wanafunzi watambue makosa kama haya. Wale ambao hawakuona mushkeli wowote katika sentensi hizi ni kuonyesha wameathrika sana kutokana na lugha ya kwanza ambayo ni Kikikuyu.

(a) Alienda hospitali kutengenezwa kichwa kilichokuwa kinamuuma.
(b) Hivyo ni kuonyeshana hukufahamu maagizo vyema.
(c) Yule kijana wa jirani anatoa kazi kwa idara gani ya serikali?
(d) Mama yule alisaidika vizuri pasipo na tatizo na mtoto alikuwa wa kiume.
(e) Halima alikuwa akipiga nguo nilipokwenda kumtembelea.
(f) Juma alipoambiwa aendelee na kazi alilalamika huku akisema alikuwa akisikia njaa.
(g) Mwalimu alimwadhibu mwanafunzi kwa kutoa nguo alizokuwa amevaa hadharani.
(h) Je, ulishika vile ulivyoambiwa?
(i) Umenionea mtoto wangu akipita hapa?
(j) Niendee na kikombe hiki nakufuata baadaye.

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY